# UHAKIKI WA MTINDO KATIKA *VIPANYA VYA MAABARA*

**NA**

**SAMUEL MWAKUYUA TSUMA**

**NAMBARI YA USAJILI: C50/75492/2012**

**NAMBARI YA SIMU: 0723170108**

**BARUA PEPE:** mwakuyuasamuel@yahoo.com

**IMETOLEWA KWA CHUO KIKUU CHA NAIROBI KAMA SEHEMU YA KUTOSHELEZA MATAKWA YA KUKAMILISHA UAMUZI WA SHAHADA YA UZAMILI**

**MWEZI WA OKTOBA 2014**

# UNGAMO

Pendekezo hili la tasnifu ni kazi yangu mwenyewe. Haijawahi kutolewa kutosheleza mahitaji ya shahada yoyote katika chuo kikuu chochote.

Sahihi: ________________________ Tarehe _______________________

JINA: SAMUEL MWAKUYUA TSUMA

NAMBARI YA USAJILI: C50/75492/2012

**Wasimamizi**

Pendekezo hili la tasnifu limewasilishwa kwa madhumuni ya kutahiniwa kwa idhini yetu kama washauri na wasimamizi tulioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi.

Sahihi: ________________________ Tarehe _______________________

PROFESA KINEENE WA MUTISO

Sahihi: ________________________ Tarehe _______________________

DAKT. AMIRI SWALEH

# TABARUKU

Safari hii ya uzamili imekuwa ya pandashuka nyingi yenye uvumilivu na makini nyingi ili kuhakikisha tumefikia mwisho wake.

Kwanza kabisa na mtabarukia mke wangu mpendwa Claris C. Lazaro kwa kuchangia kwa njia moja au nyingine. Amekuwa mfadhili kwa kujitolea kugharamia masomo yangu. Nashukuru kwa kujali masilahi na mahitaji yangu, uvumilivu aliyoonyesha katika safari hii yote, sina wakukufananisha ila nina kuombea Mola azidi kukubariki kwa vyovyote vile.

Ninawashukuru watoto wangu, wapendwa, John C. Mwakuyua (Marehemu) aliyependa elimu sana lakini ndoto yake haikutimia, Mungu amrehemu, Willy T. Mwakuyua, Edward L. Mwakuyua na Binti yangu Beatrice D. Mwakuyua kwa kuvumilia na kustahimili machungu ya kutokuwa karibu nao mara kwa mara kwa muda wa miaka miwili wakati ambapo huduma zangu kwao zilihitajika zaidi.

## SHUKRANI

Ningependa kutoa shukrani zangu nyingi kwa wale wote ambao walichangia ufanisi wa utafiti huu kwa njia moja au nyingine. Waliosema kidole kimoja hakivunji chawa hawakukosea.

Kwanza kabisa ningependa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na siha nzuri. Ameniwezesha kutimiza ndoto yangu ya kupata shahada ya uzamili katika somo la Kiswahili. Ninawashukuru wazazi wangu, Marehemu Bw. Willingtan na Bi. Beatrice D. Bakari walionizaa na kunionyesha milango ya darasa.

Ninatoa shukrani maalum kwa wasimamizi wangu, Profesa Kineene Wa Mutiso na Dakt. Amiri Swaleh kwa ushauri wao wa kitaalam na kwa kuhakikisha kuwa kazi hii imetimia. Sina cha kuwapa ila kuwaombea Mungu awape afya nzuri na maarifa zaidi. Mungu awabariki sana.

Shukrani nyingi za dhati ziwaendee wahadhiri wote wa idara ya isimu na lugha kwa ushauri walionipa na uliochangia katika kufikia malengo yangu. Shukrani maalum kwa wafuatao;Prof. Habwe mwenyekiti wa Idara ya Kiswahili kwa ushauri wake wakati wa mihadhara. Dkt. Iribe Mwangi aliyekuwa akitushughulikia na kuona kwamba masilahi yetu yanatekelezwa. Wengine ni Dkt. Mbuthia, Dkt. Zaja, Dkt. Mbatia, Bw. Mungania na Dkt. Jefwa Mweri. Mungu na awabariki sana.

Shukrani tumbi tele ziwaendee wanafunzi wenzangu tulioabiri meli moja na kuhakikisha kuwa tumefika mwisho wa safari licha ya dhoruba baharini .Hawa ni; Ruth Binyanya, Duncan Munga, Vincent Otieno, Doris Kachipela, Margaret Karanja, Sis. Teresia Waweru, Beatrice, Mariamu Ngome, Nahashon Nyangeri, Regina, Furaha Nyawa na wengine.

# UFUPISHO

K.h.j – Kama Hapo Juu

Mf.w. – Mfano

T. Y. – Tafsiri Yangu

Uk- Ukurasa

## IKISIRI

Tasnifu hii imeshughulikia uhakiki wa mtindo katika *Vipanya vya Maabara*. Tumetumia nadharia ya umuundo kwa kuwa, nadharia hii hubainisha vipengele vya kimtindo ambavyo ni tashihisi, maswali ya balagha, italiki na vinginevyo. Kufaulu kwa kazi ya kifasihi, hutokana na mbinu za kimtindo ambazo msanii amezitumia. Tumechanganua vipengele vya kimtindo katika riwaya teule. Vipengele hivi ni sintaksia, italiki, tamathali za semi na uwasilishaji wa mawazo. Tumegundua kuwa msanii amevitumia vipengele vya kimtindo kwa njia nzuri kupitisha ujumbe wake kwa hadhira.

Kazi imegawika katika sura nne. Katika sura ya kwanza, tumeshughulikia maswala ya kimsingi yanayojenga utafiti kama vile: utangulizi kuhusu mada, sababu za kuchagua somo, tatizo la utafiti, madhumuni ya utafiti, nadharia tete, msingi wa kinadharia, njia za utafiti, upeo na mipaka.

Katika sura ya pili, tumeshughulikia riwaya na uchanganuzi wa kimtindo. Tumeeleza maana ya riwaya kuwa ni hadithi ndefu iliyobuniwa na kuandikwa kwa nathari. Riwaya ni sharti iwe na migogoro, wahusika ambao ni binadamu au wanyama wachukuwao sifa za binadamu. Pia tumeeleza mtindo kuwa ni mtu, ni tabia, ni lugha na ni maisha kutegemea mawazo ya mtu binafsi.

Katika sura ya tatu, tumehakiki mtindo wa *Vipanya vva Maabara* kwa kuchanganua hasa vipengele vya kimtindo. Tumeona kuwa mwandishi amefaulu kutumia vipengele vya kimtindo na kubainisha dhamira ya kazi yake. Ameweza kupitisha ujumbe wake vizuri kwa msomaji.

Katika sura ya nne, tumetoa mahitimisho, upimaji wa nadharia tete na mapendekezo. Tumeona kuwa nadharia tete zote tatu zimetimizwa. Vipengele vya kimtindo vimetumika sawasawa katika riwaya teule. Mfano kuna uzungumzinafsia na dayalojia baina ya wahusika, tashbihi, tashihisi na nyinginezo. Msanii amefaulu kuptisha ujumbe kwa mnato kutokana na mtindo aliotumia. Ametumia maswali ya balagha, italiki, uzungumzi wa ainaaina na matumizi ya sentensi zisizokamilishwa. Tumependekeza wasomi wengine kutafiti juu ya vipengele vya kidhamira, maudhui na mengine.

## YALIYOMO

UNGAMO ii
TABARUKU iii
SHUKRANI iv
UFUPISHO v
IKISIRI vi
YALIYOMO vii
**SURA YA KWANZA 1**
1.0 UTANGULIZI 1
1.1. Tatizo la Utafiti 2
1.2 Madhumuni ya Utafiti 3
1.3 Sababu za Kuchagua Somo 3
1.4 Yaliyoandikwa Kuhusu Somo 4
1.5 Nadharia Tete 9
1.6 Msingi wa Nadharia 9
1.7 Njia za Utafiti 11
1.8 Upeo na Mipaka 12
1.9 Hitimisho 12
**SURA YA PILI 13**
RIWAYA NA UCHANGANUZI WA KIMTINDO 13
2.0 Utangulizi 13
2.1 Maana ya Riwaya 13
2.2. Maana ya Mtindo 15
2.2.1 Tashbihi 19
2.2.2 Sitiari 20

2.2.3 Tashihisi ........................................................................................ 21
2.2.4 Onomatopeia / Tanakali za sauti ................................................................ 22
2.2.5 Taharuki ........................................................................................ 23
2.2.6 Urudiaji/ Ukariri........................................................................................ 23
2.2.7 Methali ........................................................................................ 24
2.2.8 Uashiriaji ........................................................................................ 25
2.2.9 Mazungumzo........................................................................................ 25
2.2.10 Uchekeshaji ........................................................................................ 25
2.2.11 Nahau ........................................................................................ 27
2.2.12 Kirai Kitenzi........................................................................................ 27
2.2.13 Sadfa ........................................................................................ 28
2.2.14 Taswira ........................................................................................ 28
2.2.15 Balagha ........................................................................................ 29
2.2.16 Njozi........................................................................................ 29
2.2.17 Barua ........................................................................................ 30
2.2.18 Nidaa ........................................................................................ 31
2.2.19 Kuchanganya ndimi ........................................................................................ 31
2.2.20 Kejeli........................................................................................ 32
2.2.20.1 Kejeli ya maneno ........................................................................................ 32
2.2.20.2 Kejeli ya hali ........................................................................................ 33
2.2.21 Sintaksia........................................................................................ 33
2.3 Hitimisho........................................................................................ 34
**SURA YA TATU ........................................................................................ 35**
MTINDO WA VIPANYA VYA MAABARA ................................................................ 35
3.0 Utangulizi........................................................................................ 35

3.1 Dhana ya Mtindo .......... 35
3.1.1 Sintaksia ya Mapengo (Dukuduku) .......... 38
3.1.2 Italiki .......... 41
3.1.3 Tamathali za Semi .......... 46
3.1.3.1 Maswali ya balagha .......... 48
3.1.3.2 Tashbihi .......... 50
3.1.3.3 Takriri .......... 53
3.1.3.4 Tasfida .......... 54
3.1.3.5 Nidaa .......... 56
3.1.3.6 Tashihisi .......... 57
3.1.3.7 Kuchanganya Ndimi .......... 58
3.1.3.8 Methali .......... 59
3.1.3.9 Ritifaa .......... 60
3.1.4: Jinsi mawazo yanavyowasilishwa katika *Vipanya vya Maabara* .......... 61
3.1.4.1 Mtindo wa uwasilishaji halisi huru wa mawazo .......... 62
3.1.4.2 Mtindo wa uwasilishaji halisi wa mawazo .......... 63
3.2 Hitimisho .......... 64
**SURA YA NNE .......... 66**
HITIMISHO NA MAPENDEKEZO .......... 66
4.0 Utangulizi .......... 66
4.1 Muhtasari wa Matokeo .......... 66
4.2 Upimaji wa nadharia tete .......... 68
4.3 Mapendekezo ya utafiti zaidi .......... 69
**MAREJELEO .......... 70**

# SURA YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

Utafiti wetu unahusu mtindo katika riwaya ya *Vipanya vya Maabara* ya Mwenda Mbatiah. Katika sura hii tumeangazia maswala ya kiutangulizi ya utafiti. Mambo tunayoyazingatia ni tatizo la utafiti, madhumuni ya utafiti, nadharia tete, mbinu za utafiti, umuhimu wa utafiti, upeo na mipaka, yaliyoandikwa kuhusu mada na uhitimisho wa sura.

Riwaya ya *Vipanya vya Maabara* (Mbatia, 2007) inajitokeza kama kazi ambayo imeangazia kabisa matatizo yanayowakumba vijana katika jamii na pia mchango mkubwa ambao vijana wanaweza kutoa suluhisho ya baadhi ya matatizo kama ukabila. Ingawa mazingira ambayo yamechukuliwa kama mandhari ya jiji la Nairobi na viunga vyake, matatizo na changamoto ambazo zinawakumba vijana kama Bob Kerogo, Wairi, Swaleh na Muli ni hakikisho zuri sana la hali ya vijana katika taifa letu kwa jumla. Mwandishi kwa namna ambayo hajaieleza bayana hapo awali anatufanya kuona ni kwa nini vijana wanakumbwa na matatizo chungu nzima. Muli anabugia dawa za kulevya kwa ajili ya kukosa baba mzazi wa kumwelekeza.

Bob na Freda wanasoma kwa taabu sana kwa sababu ya ulevi wa baba yao anayekata tamaa kwa sababu ya kutopandishwa cheo kazini. Wairi anakosa mwelekeo kwa sababu wazazi wake hawana nafasi ya kumwelekeza. Muda wao mwingi wamo katika harakati za kutafuta pesa. Hata mfumo wa elimu unachangia matatizo yanayowakumba vijana. Jamila kwa mfano anaenda chuo kikuu cha Egerton kusomea shahada ya B.Sc ilhali moyo wake ulitamani uhandisi.

Riwaya hii imebeba uhalisia kamili kwa sababu imeandikwa katika nafsi ya kwanza ambayo inatufanya kuhisi uyakinifu wa matukio yote. Kwa mfano: *Niliinuka, nikambusu wairi shavuni ili kumchangamsha* (uk. 191).

*Vipanya vya maabara* ni riwaya inayoangazia maisha hasa ya vijana katika muktadha wa hali ngumu kiuchumi na hata kisiasa wakati wa miaka ya themanini na tisini. Huu ni muda ambapo taifa la Kenya lilikumbwa na ufukara, ufisadi, uozo wa kimaadili na kufilisika kwa asasi za kielimu, kiafya na kiuchumi.

Mwandishi anamchora Bob kama kijana mwenye bidii za mchwa na kuwa kielelezo bora kwa vijana wengine. Kupitia kwa Bob inadhihirisha kwamba jitihada huondoa kudura kwani alikuwa habagui kazi, aliosha magari, akafanya kibarua kwa wahindi kupanga vitabu na mwisho akawa na bahati ya mtende.

**1.1. Tatizo la Utafiti**

Tatizo la utafiti huu lilikuwa kuhakiki mtindo katika *Vipanya vya Maabara*. Mtindo hujumuisha vipengele muhimu ambavyo huipa kazi ya kisanaa sifa mahususi. Vipengele vya kimtindo pia vina ushirikiano na uhusiano mkubwa katika kupitisha ujumbe uliokusudiwa katika kazi ya kisanaa. Fauka ya hayo, matumizi mwafaka ya vipengele mbalimbali vya kimtindo huifanya kazi ya fasihi kuwa na mnato, mvuto na uzuri wa kipee. Hata hivyo, matumizi mabaya ya mtindo hupelekea kazi ya kifasihi kukosa usanii na hata uzuri wake, yaani huwa chapwa na huathiri namna ujumbe unavyomfikia msomaji.

Msanii yeyote anapokata shauri kuchagua vipengele fulani vya kisanaa sharti viweze kuvutia hadhira, kuchokonoa na kuathiri hisia zao. Mtindo unakuwa ni kigezo cha kupimia kufaulu au kutofaulu kwa msanii katika usanii wake. Mtunzi wa riwaya huhitaji weledi wa hali ya juu ili kuweza kufikia upeo wa ubunifu wake.

## 1.2 Madhumuni ya Utafiti

Madhumuni ya utafiti huu ni kuhakiki mtindo katika riwaya ya *Vipanya vya Maabara*. Katika uhakiki huu tunakusudia kufanya yafuatayo:

*i.* Kubainisha na kuchanganua vipengele mbalimbali vya kimtindo ambavyo vimetumika katika *Vipanya vya Maabara.*

*ii.* Kutathmini mchango wa vipengele vya kimtindo katika kuwasilisha ujumbe katika *Vipanya vya Maabara.*

iii. Kutathmini kufaulu au kufeli kwa mtunzi kwa kutumia ya baadhi ya vipengele vya kimtindo katika riwaya yake.

## 1.3 Sababu za Kuchagua Somo

Mwandishi wa Riwaya ya *Vipanya vya Maabara*ni Mwenda Mbatia. Mbatiah ameandika riwaya ya *Upotevu* ambayo imeeleza maswala ya kijamii. Hivyo basi, utunzi wake mzuri wa kuipamba lugha ambao uimewezesha kupitisha mawazo yake kwa njia ya kusisimua.

*Vipanya vya Maabara* ni riwaya inayoangazia hali ya vijana wanaokumbwa na wimbi la mabadiliko ya kisiasa, kiuchumi na kuporomoka kwa asasi za kijamii, kama hospitali, elimu na kilimo. Tumechagua kushughulikia *Vipanya vya Maabara kimtindo kwa kuwa*

haijashughulikiwa. Uhakiki ambao mpaka sasa umefanywa ni wa Naliaka[2012] . Ametumia nadharia ya uhalisia.Alisema kuwa vijana wanatumiwa na wanasiasa kutenda maovu.Aliwalinganisha vijana na panya katika maabara,kwani ndiyo waumiao.Upungufu wake ni kwamba hakuweza kutoa suluhisho mwafaka kwa vijana ili waweze kuishi maisha mema. Sisi tutajikita katika kuchunguza vipengele vya kimtindo, tukitumia nadharia ya umuundo.

Tulichagua kutafiti mtindo katika kazi hii ili kuona ulivyochangia kujenga dhamira za mwandishi na kuacha athari kwa msomaji. Aidha, tuliona ni bora kuchagua kipengele cha mtindo kutathmini ubora au udhaifu wa matumizi hayo katika riwaya teule. Hii itatuwezesha kutathmini kufaulu au kufeli kwa mwandishi wa *Vipanya vya Maabara*katika uteuzi na matumizi yake ya mtindo.

**1.4 Yaliyoandikwa Kuhusu Somo**

Tumegundua kuwa hakujafanywa utafiti wowote wa kimtindo kuhusu *Vipanya vya Maabara*.

Kirumbi (1975) anadai kuwa nyimbo nyingi huwa na matumizi ya tamathali za semi. Japo hoja zake ni kuhusu fasihi simulizi na yetu ni kuhusu fasihi andishi, basi tumeweza kusema kwamba, hata fasihi andishi na hasa riwaya huchukua nafasi kubwa katika maisha ya watu. Hivyo basi, hoja zake ni kweli hasa katika utafiti wetu ambapo tunachunguza matumizi ya tamathali za semi katika *Vipanya vya Maabara* ambazo ni baadhi ya vipengele vya mtindo.

Mazrui (1981), anaainisha vipengele vya uchambuzi wa riwaya kwa jumla na kuonyesha vipengele vya mtindo ambavyo mchambuzi wa riwaya angetumia katika shughuli yake hiyo. Mazrui alichanganua tamathali za semi, ploti, wahusika na zinginezo. Kinyume na Mazrui, sisi tumechambua riwaya moja tu *Vipanya vya Maabara* tukijikita zaidi katika mtindo wake. Hata hivyo, mwongozo wake umetusaidia sana kubainisha vipengele mbali mbali vya kimtindo,mfano tashibihi, muundo wa sentensi na tamathali za semi.

Marwa (1987), katika tasnifu yake anatumia nadharia ya Mcintosh kuchambua tofauti au ulingano wa mtindo baina ya ngano za Waswahili na Wakuria. Kwamba mtindo ni jinsi mtu anavyozungumza kila siku, ikiwa anatazama au hatazami, akijaza makosa au bila kujaza makosa (kufanya makosa au bila kufanya makosa).Hii inaonyesha jinsi vile mtu anavyozungumza au kujieleza kimaandishi kuwa ni mtindo .Mcintosh, kwake hakuna sarufi mbaya. Mchango wa Marwa umetufaa sana katika uchambuzi wa mtindo katika riwaya. Jambo linalojitokeza ni kwamba, mtindo huandamana na lugha. Kwa hivyo, mahusiko yetu juu ya mtindo yanakuwa ni kuangalia lugha anayoitumia mwandishi wa *Vipanya vya Maabara* kuupitisha ujumbe kwa wasomaji.

Mlacha na Madumulla (1991), wanashughulikia historia, nadharia, swala la dunia na uchanganuzi wa riwaya kwa ujumla. Wamejaribu kuonyesha njia tofauti na zinazotumika kuchambua riwaya na pia wameonyesha jinsi uhakiki wa riwaya ulivyo tata na ambao umehitaji mhakiki kuwa thabiti zaidi. Mawazo yao kuhusu uchambuzi yametufaa sana katika uchambuzi wetu wa mtindo katika *Vipanya vya Maabara*.

Omwoyo (1997), anashughulikia fani katika ushairi wa Hassan Mwalimu Mbega. Amehakiki *Upisho wa Malenga na Dafina ya Malenga.* Ametumia nadharia ya urasimu. Utafiti wake ulionyesha kwamba, fani ina mchango mkubwa katika kufumbata malengo ya msanii. Amesema fani ni kipengele muhimu sana cha fasihi.

Tofauti na utafiti wake, tumezamia zaidi katika uhakiki wa mtindo katika *Vipanya vya Maabara* kwa kutumia nadharia ya umuundo. Utafiti wa Omwoyo umetufaa sana kubainisha vipengele vya mtindo katika riwaya teule.

Mbatiah (1999), anatafiti riwaya ya tasnifu. Anasema kwamba maelezo ya neno *tasnifu*, inamaanisha wadhifa, tatizo, hoja au wazo ambalo linahitaji kutetewa au kujadiliwa. Ameendelea kusema kuwa riwaya ya tasnifu inaendeleza au kutetea tasnifu fulani kwa umakini zaidi. Riwaya tasnifu imefafanuliwa na Holman (1972:576) kama ifuatavyo:

> Ni riwaya ambayo inachunguza baadhi ya maswala ya kijamii, kiuchumi, kisiasa ama ya kidini ambayo yanatoa maoni ya kitasnifu yaliyo na suluhisho (T Y).

Mawazo ya Mbatiah kuhusu riwaya yametusaidia kufahamu riwaya tasnifu, ambayo huwa inatoa suluhisho ya matatizo.Kwa mawazo haya, tumeweza kujua kwamba lazima mitindo mbalimbali ya uwasilishaji wa mawazo yatumike. Hivyo basi huweza kuchanganua mitindo hiyo. Mtindo ndicho kipengele cha utafiti wetu.

Kisilu (2003), anatafiti mwingiliano wa fani na maudhui katika ushairi wa Kithaka wa Mberia. Alijikita kwenye diwani za *Mchezo wa Karata* (1997) na *Bara Jingine* (2001). Ametumia nadharia ya umuundo. Ameorodhesha kunga za tashbihi, takriri, sitiari, taashira, maswali ya balagha na msisitizo bayana. Japo mawazo yake yameegemea

ushairi, tofauti na utafiti wetu, unatusaidia sana. Vipengele vya kimtindo vina mchango mkubwa katika uundaji wa maudhui.

Wamitila (2003), anasema kwamba, dhana ya mtindo hurejelea jinsi ya kujieleza katika kazi ya kifasihi. Amezidi kusema kuwa tunaweza kuueleza mtindo kama jinsi mwandishi fulani anavyojieleza katika kazi yake. Uchunguzi wa mtindo unahusisha kuangalia uteuzi wa msamiati, tamathali za usemi, mbinu za kibalagha, miundo ya sentensi, sura na upana wa aya zake pamoja na uakifishi wake. Hivyo basi, mawazo ya Wamitila yanaenda sambamba na utafiti wetu kwani tunachunguza matumizi ya baadhi ya vipengele vya kimtindo kama tashihisi, italiki, tamathali za semi na tashbihi katika *Vipanya vya Maabara*. Maoni yake yametufaa na yametuwezesha kuelewa baadhi ya vipengele vya kimtindo katika kazi za fasihi na hasa riwaya tunayoishughulikia. Kwa maoni yetu mtindo ni vazi la usanii avaalo msanii binafsi.Vazi hilo humtofautisha na msanii mwingine,kwani huwa ni la kipekee.

Swaleh (2011), anatafiti *umbo* na mitindo ilivyotumika katika Usawiri wa Uana na Mamlaka kama mfumo mahususi wa kuelezeka. Amesema kwamba muundo na mtindo unaotumiwa na mwandishi, haunauhusiano wamoja kwa moja katika ujenzi wa ujitambuzi na utambulisho wa jinsia katika riwaya teule. Mawazo yake yametufaa kwani, tumejua kwamba waandishi hutumia mitindo tofauti tofauti kuwasawiri wahusika jambo linaloathiri utambulisho wao katika jamii. Hata hivyo kazi yetu ni kuhakiki baadhi ya vipengele vya mtindo katika *Vipanya vya Maabara*.

Mugwika (2012), katika tansifu yake akiongozwa na nadharia ya Urasimu wa Kirusi, anahakiki dhana ya uchimuzi katika uendelezaji wa riwaya ya kimajaribio ya *Mafamba*. Anasema kwamba, mtunzi ametumia mitindo tofauti ya lugha inayoyachimuza mambo tofauti kufanya yaonekane wazi katika uwasilishaji wa maudhui kwa njia yenye kuathiri. Katika kazi yetu tumechunguza jinsi mtunzi ametumia mitindo mbalimbali ya lugha kuchimuza mambo iliyaonekane wazi saidi katika *Vipanya vya Maabara*. Mawazo ya Mugwika yametusaidia katika kuonyesha ni vipengele gani vya mtindo vinakuwa muhimu katika kuupa ujumbe mnato.

Mboti (2012) Akimnukuu Kingei (1992) ambaye ameshughulikia lugha, utamaduni na mawasiliano katika nyimbo za taarabu nchini Kenya kati ya mwaka 1963-1990. Utafiti wake umetufaa kwa kuwa umetupa mwelekeo kuhusu vipengele vya lugha na hasa tamathali za semi katika kuchambua *Vipanya vya Maabara*. Japo utafiti wake ni tofauti na wetu. (Mboti ametafiti lugha utamaduni na mawasiliano katika lugha). Sisi tumechanganua vipengele vya mtindo.

Manoti (2012) katika tasnifu yake anahakiki dhamira ya uozo na athari zake kwa jamii katika riwaya ya *Upotevu*, akitumia nadharia ya maadili. Anasema mwandishi amefaulu katika kuwasawiri wahusika wema na waovu kuwakilisha wema na uovu katika jamii. Tofauti na utafiti wake, tunachunguza mtindo katika *Vipanya vya Maabara*. Mawazo yake yametufaa kwa kuwa wahusika katika riwaya ni muhimu katika kuendeleza dhamira ya mwandishi. Pia wahusika ni kipengele kimoja  wapo cha mtindo.

Naliaka (2012) anatumia nadharia ya uhalisia kuhakiki *Hali ya vijana katika riwaya ya Vipanya vya Maabara*. Matokeo ya utafiti wake ni kwamba, vijana wanatumiwa na wanasiasa wakwasi ili kuzua fujo. Aidha, vijana kwa kuwa wanapewa fedha ili watende maovu kama kuuwa, kuiba na maovu mengine katika jamii. Amefaulu kwa kuwapanga wahusika vijana katika matapo tofauti ya wazuri na wabaya.

Kwa kiwango kikubwa kazi yake imetuchochea katika kuichanganua riwaya teule ambayo ndio msingi wa mada yetu.

**1.5 Nadharia Tete**

Kazi yetu itaongozwa na nadharia tete zifuatazo:

i. Vipengele vya kimtindo vilivyotumika katika *Vipanya vya Maabara* vimechangia pakubwa katika uwasilishaji wa maudhui.

ii. Msanii wa *Vipanya vya Maabara* amefaulu kupitisha ujumbe kwa mnato kutokana na mtindo alioutumia.

iii. Msanii amefaulu au amefeli kutumia baadhi ya vipengele vya kimtindo katika riwaya yake.

**1.6 Msingi wa Nadharia**

Uhakiki wetu umetumia nadharia ya umuundo. Umuundo uliibuka nchini Czcheslovakia mwishoni mwa miaka ya ishirini. Nadharia ya umuundo iliasisiwa na Roman Jakobson. Trubetzkoy, Jan Mukarovsky, Buris Tomaserky. Roman Jakobson alikuwa amehama Ujerumani baada ya kupigwa marufuku kwa urasimu nchini Urusi. Wasomi hawa

walibuni kundi lililojulikana kama shule ya isimu ya Prague na wakaitumia kuendeleza mawazo yao.

Kama anavyoelezea Culler (1995:4-5) waasisi wa umuundo walitumia mawazo ya mwanaisimu Ferdinand de Saussure ambaye alibuni dhana mabalimbali za kiisimu na akawafundisha wanafunzi wake wakiongozwa na Charles Bally katika *A Course in General Linguistics* (1916).

Ferdinand de Saussure alibuni na kufafanua dhana za *Langage* (Lugha ijulikanavyo na kutumiwa na jamii), *Langue* (sheria za kanuni za lugha) na *Parole (*Matumizi ya lugha katika mazungumzo na maandishi). Wanamuundo walitumia dhana hizi kusisitiza kuwa, ili kuelewa mfumo wa kazi ya kifasihi, mhakiki anafaa kuchunguza matumizi ya lugha katika maandishi au mazungumzo, vipengele vyake na mahusiano yake. Wanaumuundo walieleza kuwa fasihi ni mfumo unaojisimamia kama *Langue* na una faida zake. Hivyo basi, kazi ya kifasihi inafaa kuangaliwa kwa mujibu wa kanuni bia za utanzu zinazoitawala.

Waasisi wa umuundo walitumia dhana za Saussure za kiashiria na kiashiriwa na wakaeleza kuwa, lugha huundwa kwa viashiria na viashiriwa. Wanamuundo wanaviona vipengele vya fani kama viashiria. Maana inayotokana na vipengele hivi vya kimtindo ndivyo viashiriwa.*Sasa tulijikuta kama vifaranga ambavyo mama yao ameshatwaliwa na nguchiro* (uk. 164). Hii ni tashibihi na ni kipengele cha mtindo. Maana ya tashbihi hii ni

kuwa inatuchorea taswira ya familia ya Konstebo Kerogo, walivyohisi baada ya baba yao kuaga dunia.

Waasisi wa umuundo walihakiki mashairi na tungo nyingine za kifasihi. Walichunguza upatanifu wa sauti, vina, mizani, kiimbo, wizani na arudhi kwa jumla. Kwa upande wa tungo za kimasimulizi walisisitiza umbo la msuko, hadithi na umbaji wa wahusika. Walichunguza pia mbinu za kimtindo kwa mfano matumizi ya jazanda, taswira, tashihisi, sadfa na ukiushi. Walieleza kuwa matumizi ya hali ya juu ya mbinu hizi huitofautisha lugha ya kifasihi na lugha ya kawaida na taaluma nyinginezo. Sisi tumetumia nadharia ya umuundo kubainisha vipengele vya mtindo ambavyo ni tashihisi, maswali ya balagha, italiki, tashbihi na vinginevyo.

Wanamuundo wanasema kuwa kufaulu kwa kazi ya kifasih,i hutokana na mbinu za kimtindo ambazo msanii amezitumia. Wanaamini kuwa uhakiki wa kazi ya kifasihi haufai kuwa na urejelezi wa nje. Umuundo wanazingatia zaidi muundo wa kazi ya kifasihi kuliko mandhari ya kijamii ya kazi hiyo. Hupuuza kuihusisha fasihi na mtunzi wake. Nadharia hii imetufaa katika uhakiki wa vipengele mbalimbali vya kimtindo katika *Vipanya vya Maabara* ili kuuweka ujumbe wake wazi zaidi.

**1.7 Njia za Utafiti**

Tumesoma riwaya teule kwa mapana na marefu. Tumesoma nadharia ya umuundo na kuzijua sifa zake na jinsi vipengele vyake vinavyotumika katika uchambuzi na uhakiki wa riwaya. Tumedurusu tasnifu za watafiti wengine ambazo zinaangazia mtindo na zilizo

na ukuruba fulani na utafiti wetu. Tumesoma vitabu vya uhakiki ilitupate mwongozo wa jinsi ya kuchanganua riwaya kitindo. Hatimaye, tuliwahusisha wasimamizi wetu na wasomi wengine katika mijandala ili kujinoa kwa jukumu lililotukabili.

### 1.8 Upeo na Mipaka

Utafiti huu umehusu uhakiki wa mtindo katika *Vipanya vya Maabara*. Utafiti wenyewe umeangazia tashbihi, tashihisi, italiki kama vipengele vya mtindo vilivyotumiwa na mwandishi kuwasilisha ujumbe wake. Mtindo ni kipengele cha fani ambacho kinakuwa kiungo muhimu katika riwaya. Matumizi mazuri ya vipengele vya kimtindo, huipamba riwaya na kuufanya ujumbe unite. Tumeshughulikia tamathali za usemi, sintanksia, njia za uwasilishaji wa mawazo, italiki, nidaa, tasfida, methali, takriri, tashihsi, kuchanganya ndimi na ritifaa.

### 1.9 Hitimisho

Katika sura hii tumejadili maswala ya kiutangulizi ya utafiti. Tumeangazia tatitzo la utafiti, madhumuni ya utafiti, sababu za kuchagua mada, yaliyoandikwa kuhusu mada, nadharia tete, msingi wa nadharia, njia za utafiti, upeo na mipaka na hitimisho. Sehemu hii ndiyo kurunzi katika utafiti huu.

## SURA YA PILI

## RIWAYA NA UCHANGANUZI WA KIMTINDO

### 2.0 Utangulizi

Sura hii inaieleza maana ya riwaya ya Kiswahili .Tmewarejelea baadhi ya wasomi na mawazo yao kuhusu utanzu huu. Kisha tumeeleza mitindo mbalimbali ya uandishi wa riwaya itumiwayo na waandishi ili kuboresha kazi zao.

Tumehiari kueleza mtindo wa riwaya kwa kuwa utafiti wetu ni kuhakiki baadhi ya vipengele vya mtindo katika *Vipanya vya Maabara*.

### 2.1 Maana ya Riwaya

Kamusi ya Kiswahili Sanifu toleo la tatu inaeleza maana mbili za neno *riwaya*. Maana ya kwanza ni kwamba *riwaya ni hadithi ndefu ya kubuni iliyoandikwa kwa maandishi ya nathari, aghalabu inayoeleza ukweli fulani wa maisha.* Maana ya pili ya riwaya ni *nadharia tofauti za elimu kutokana na wataalamu au wanazuoni mbali mbali kuhusu jambo fulani.Utfiti wetu* utatumia maana ya kwanza ya riwaya inayoelezewa

Wamitila (2003) anaieleza riwaya kama hadithi ndefu ambayo ina visa na vitushi, migogoro na inayosimulia mambo yanayo husiana na jamii. Riwaya ni kazi ya kubuni na huhusisha binadamu au wanyama (wahusika) ambao wanatenda mambo fulani kwa ukamilifu fulani na matukio yake huhusisha kipindi au wakati fulani. Katika riwaya huwa kuna mambo kadha wa kadha ya kuangalia kama dhamira na maudhui, wahusika, migogoro na mivutano, muundo na mtindo na mandhari.

Wamitila (k.h.j.) anazidi kutuelezea ya kwamba, riwaya ni kazi ya kinathari au kibunilizi ambayo huwa na urefu wa kutosha. Lakini urefu wa kutosha ni upi? Riwaya inapaswa kuwa na msuko uliojengeka vizuri na ambao unaonyesha vitushi mbalimbali.

Aghalabu wahusika wa riwaya huwa wengi na walioendelezwa kwa kina. Kazi yenyewe huchukua muda mrefu na mandhari huwa na mchango mkubwa kuliko ilivyo katika novela na hadithi fupi. Kazi nyingi za kinathari za kifasihi zinaakisi baadhi ya sifa hizi lakini si *Rosa Mistika,Nagona na Mzingile* riwaya za Kezilahabi, zina upana wa kiwakati na uchangamano wa kimaudhui lakini ni fupi. Uzito, upana na uchangamano wa maudhui, kina cha uhusika na mandhari,zinatosha kuainisha kazi hizi kama riwaya ijapokuwa idadi yake ya maneno si kubwa sana.

Kulingana na Mazrui na Syambo (1992)  riwaya ni utungo wowote mrefu wa hadithi yenye ploti na iliyobuniwa kwa maandishi ya nathari. Lakini utungo mpaka uwe na urefu gani ndipo uitwe riwaya? Swali hili bila shaka ni vigumu kujibika kwa sababu dhana yenyewe ya urefu wa utungo inategemea maendeleo ya fasihi katika jumuiya mbalimbali. Kwa mfano, nyingi katika tungo tunazoziita riwaya katika fasihi ya Kiswahili ni fupi mno tukizilinganisha na zile za kimagharibi, lakini wakati huo huo ni ndefu mno kuliko ngano na hekaya za fasihi – simulizi.

Zaidi ya urefu wa utungo, riwaya ni lazima iwe hadithi ya kubuniwa yenye ploti. Hadithi ni mpangilio wa matukio mbalimbali katika muhula maalum kama “kulitokea jambo A, likafuatiwa na B, halafu likaja C, na mwishowe likatokea D”. Ploti kwa upande

mwingine inahusiana na uhusiano uliopo baina ya matukio haya na namna tukio moja linavyosababisha jingine.

Tumedai pia kwamba riwaya kwa kawaida hubuniwa kwa maandishi ya nathari. Urefu wa riwaya, muundo wake na mchanganyiko wa mbinu zake za kisanaa, ni mambo yanayozifanya tungo za utanzu huu zisiweze kutungika bila maandishi. Na maandishi haya ni lazima yawe ya nathari, yaani ya insha ya usimulizi wa moja kwa moja, ingawa hapa na pale katika riwaya tunaweza kupata vipande vya ushairi, wimbo au lugha ya mazungumzo.

Dunia ya riwaya nyingi ni dunia ambayo imekaribiana zaidi na hii yetu. Kwa kawaida watu wake huwa ni kama sisi, tamaduni zake huwa ni kama zetu, matukio yake huwa ni ya kuaminika kama yale ya ulimwengu wetu, jumuiya zake zina mifumo tunayoweza kuitambua.

## 2.2. Maana ya Mtindo

McIntosh (1963:243) anasema kuwa mtindo kama njia ya kujieleza, sio tu vile waandishi wanavyojieleza, lakini pia ni vile watu mbalimbali wazungumzavyo ama waandikavyo matukio tofautitofauti kila uchao. Kwa hivyo mtindo ni vile tujielezavyo natufanyavyo katika maisha. Mambo tuyafanyayo na tuyazungumzayo, huweza kubainisha hulka zetu na kuwa mtindo. Mtindo huo hututofautisha na wenzetu ambao huwa na mitindo yao ya kipekee.

Crystal na Davy (1969:9-10), wana umimtindo hao wanasema kuwa, mtindo hurejelea baadhi ama tabia zote za lugha za mtu binafsi, ama tabia zote za lugha walizonazo watu katika kundi Fulani. Vivyo hivyo zinaweza kuwa tabia za lugha za kikundi fulani walizoshirikiana kwa kipindi maalum. Kwa hiyo, wasomi hawa wanachotaka kusisitiza ni kuwa, mtindo hurejelea mazowea ya mtu katika matumizi ya lugha.

Hoja hii ni ya kweli kwani lugha hudhihirisha matabaka mbalimbali ya watu. Kwa mfano, wakazi wa Nairobi, japo si wote, hupenda kuzungumza kingereza. Lakini mtu wa kutoka mashambani Malindi, huzungumza aidha Kigiriyama ama Kiswahili. Kwa hivyo watu hawa wawili wakiwa pamoja, ni rahisi kuwafahamu. Yule mkazi wa Nairobi atazungumza kingereza ili aonekane kuwa ni bora kuliko mwenzake. Kwa hivyo mtindo ni lugha. Mfano mwingine ni wa kisiasa. Huweza kujua mazungumzo ya mwanasiasa mmoja kutoka kwa mwingine, kwa kusikiliza maongezi yake. Raila hujulikana sana kwa kuanza hotuba zake kwa vitendawili ama mafumbo. Kwa hivyo huu ni mtindo wake wa lugha kwani ameuzowea. Tuseme kwamba kila binadamu ana mtindo wake wa lugha. Vile azungumzavyo na aandikavyo katika maisha, humdhihirisha mtu vile alivyo kilugha.

Kitsao (1975) anaorodhesha baadhi ya mitindo itumiwayo na watu miongoni mwao wasanii. Mbinu hizo ni pamoja na mtindo ni mtu, mtindo kama mazowea ya lugha, , mtindo kama njia ya kujieleza na mtindo kama chaguo la mtu.

Mawazo ya Kitsao ni mazuri kabisa, lakini hata hivyo, kuna aina nyingi za mitindo ambayo mtu ama msanii hutumia. Tuseme kuwa wasanii wengine hupenda kuandika sentensi fupi fupi, sentensi ndefu ndefu na wengine hupenda kumalizia ibara kwa methali au msemo. Hiyo ni mitindo yao. Kwa hiyo tuseme kuwa mtindo ni vile mzungumzaji au mwandishi atumiavyo maneno, apangavyo sentensi zake na atendavyo shughuli zake kila siku. Mambo ayafanyayo kila uchao kwa muda mrefu na ya kiwa yanafanana, basi yanakuwa ni mtindo wake. Dhana ya mtindo ni pana sana, lakini itategemea kigezo cha msanii mwenyewe.

Kila mwandishi ana mtindo wa lugha yake mahususi. Lugha ambayo huonekana katika kazi zake zote. Lugha ambayo inamtofautisha na lugha za waandishi wengine. Ubinafsi wa mwandishi wapaswa udhihirishwe kutokana na mtindo wake wa uandishi. Kwa kauli nyingine mtindo ni kiwiliwili cha mwandishi. Kazi zake ndizo hubainisha ubinafsi na upekee wake katika ulingo wa (fasihi).

Maoni yetu ni kwamba, mtindo wa mwandishi mmoja huwa tofauti na mtindo wa mwandishi mwingine. Kwa hivyo tungependa kusema kuwa, mtindo ni joho la mwandishi. Joho hilo hulivaa na humtofautisha na majoho yavaliwayo na waandishi wengine.

Kuipa nguvu hoja hii, ni kuwa, mtindo wa uandishi wa daktari Habwe ni tofauti kabisa na mtindo wa uandishi wa daktari Wamitila. Tofauti zao zipo kwenye matumizi ya vitushi vya lugha. Wamitila hutumia sana viungo vya lugha, ilihali Habwe huvitumia viungo hivyo kwa wastani.

Mawazo yetu ni kwamba mtindo ni chaguo la mtu. Msemaji ama mwandishi huteua maneno ambayo angependa kuyasema ama kuyaandika. Uteuzi huo huhitaji umakinifu, ni kutokana na uchaguzi mzuri wa maneno ambayo mwandishi angependa kuyatumia, ili kazi yake ipendwe. Kwa hiyo mwandishi huchagua maneno, muundo wa sentensi, tamathali za lugha, ambazo kwazo huonekana katika kazi zake zote. Ikiwa hivyo basi hudhihirisha kuwa mtindo ni chaguo la mtu.

Indangasi (1988) anazungumzia juu ya elimu–mitindo. Anajadili historia ya elimu–mitindo na sehemu za kuchunguza mtindo ambazo ni: sintaksia, fonolojia, msamiati, sentensi pamoja na tamathali za usemi. Maelezo haya yameonyesha kuwa mtindo huweza kuwa fonolojia, sintaksia, semantiki, msamiati ama tamathali za usemi. Hivyo basi mtu ama msanii husema fonolojia kama mtindo wake na wengine waseme vipengele vingine kama mitindo yao.

Msokile (1992) anasema kuwa mtindo ni kama mtu mwenyewe. Anaendelea kusema kwamba mtindo ni kama tabia ya uandishi katika kipindi fulani cha mfumo fulani wa maisha ya mtu. Anaorodhesha baadhi ya vipengele vya mtindo ambavyo ni: uchaguzi na maneno, matumizi ya taswira na ishara, maelezo na masimulizi.
Mawazo haya yametufanya tusema kuwa mtindo umechukua nyenzo zote za uandishi ambazo mwandishi angezitumia. Baadhi ya nyenzo hizo ni tamathali za lugha, maneno, sentensi, maelezo na masimulizi. Hivyo basi mtindo ni tabia na ni mtu mwenyewe.

Mohamed (1995) anaeleza na kuchambua maana ya mtindo. Anaangalia aina mbali mbali za mtindo kama: mtu mwenyewe, mtindo kama nyenzo zinazobwia wazo kuu, mtindo kama jumla ya tabia za lugha za kikundi au wakati fulani na mtindo kama kuukimbia ukawaida. Kutokana na mawazo haya, tuseme kwamba mtindo ni mtu mwenyewe, ni lugha, ni tabia na ni ukimbiaji wa ukawaida.

Okondo na Wachira (2006:68) wanasema kwamba, mbinu za uandishi ni maneno au mafungu ya maneno katika sentensi ambayo mwandishi ametumia katika kazi zake. Msanii hufanya hivyo ili kazi iwe ya kuwavutia wasomaji na wasikilizaji. Wanazidi kusema kuwa, waongezapo viungo vya uandishi katika hadithi, basi itajibainisha wazi kuwa ni mtindo wa kipekee. Mbinu hizi husaidia kuwasilisha toni, maana na maudhui kwa wasomaji. Kwa maoni yetu, mbinu za uandishi ni ufundi wa utumiaji maneno au fungu la maneno, sentensi, aya, sura katika riwaya nzima. Ufundi huu humwezesha msanii kuwasilisha mawazo yake vema kwa hadhira lengwa.

Kuna mbinu nyingi zitumiwazo na wasanii kupitisha ujumbe wao kwa njia ya kupendeza na kuwanasa wasomaji. Mbinu hizi ni pamoja na tashibibi, Sitiari, tashihisi, onomatopeia au tanakali za sauti, taharuki, methali, uashiriaji, mazungumzo, uchekeshaji,nahau na kirai kitenzi.

### 2.2.1 Tashbihi

Ni hali ya kumchorea mtu picha akilini juu ya kitu kimoja au zaidi kwa kuvilinganisha[T.Y]. Tashbihi ni usemi wa ufananisho au mlinganisho wa vitu viwili au zaidi. Kawaida vitu vinavyolinganishwa huwa si vya aina moja au muundo mmoja.

Tashibihi hutumiwa ili kumwezesha msomaji kuwa na uelewa wa kina wa ujumbe ausomao.

Vivyo hivyo, tashibihi humsaidia mwandishi kusisitiza ubora fulani wa ujumbe katika maandishi. Pia,humfanya mwandishi kutoa ujumbe wazi kwa kulinganisha au ulinganishaji.

Kwa maoni yetu, tumeona kuwa mbinu ya utumiaji wa tashibihi katika riwaya, humwezesha mwandishi kuchora taswira katika ubongo wa msomaji. Kwa hali hii basi, kumfanya anaswe na hadithi na kumwathiri kifikra.Tashibihi hubainishwa kwa matumzi ya maneno kama vile mithili ya, mfano wa,sawa na, kama na kuadhalika.

Mfano wa tashbihi

i. Fatuma ni mfupi kama mbilikimo-Kumaanisha Fatuma ni mfupi sana.
ii. Beberu wetu haoni mithili ya jongoo-Beberu haoni kabisa,kwani jongoo hana macho.
iii. Mwalimu wetu wa somo la Kiswahili ni mnene sawa na mbuyu-Yaani mwalimu ni mnene sana.
iv. Ugali ulio pikwa jana ulikuwa mweusi kama vile lami-Ugali ulikuwa mweusi.
v. Mzee Chausiku ni mrefu ja ngamia-Mzee Chausiku ni mrefu.

### 2.2.2 Sitiari

Sitiari hutumiwa kuonyesha uwiano uliopo kati ya vitu viwili au zaidi vilivyo tofauti kabisa.Ni uelezaji wa kitu kimoja kutoka kwa kingine bila matumizi ya viungo; Kama mithili ya,kama vile na mfano wa.Kiunganishi [ni]ndicho hutumiwa.Katika sitiari

mfananisho huwa ni wa mdokezo,lakini kwa upande wa tashbihi ulinganishi huelezwa au huwa kwa maelezo.

Sitiari hutumiwa na waandishi kwa madhumuni mbalimbali. Baadhi ya madhumuni hayo ni kuonyesha tabia ya mtu au kitu, kutoa ukweli wa jumla, kuongeza uelewaji wa ujumbe fulani na kuifanya matini isomwayo kuwa hai. Mifano ya sitiari ni kama vile;

(i) Lazaro ni simba. Kumaanisha Lazaro ana ujasiri kama simba.

(ii) Baba ni jiwe. Kumaanisha baba ni mgumu aidha wa kutumia pesa.

(iii) Bakari ni simaku. Inamaanisha Bakari ni mwepesi wa kushika na kuelewa mambo.

(iv) Chakula kilichopikwa juzi kilikuwa ni asali.Kumaanisha chakula kilikuwa kitamu.

### 2.2.3 Tashihisi

Tumeeleza tashihisi kuwa ni njia moja wapo ya uandishi yenye kuipa vitu visivyo kuwa na hisi kuweza kuhisi.

Tashihisi ni mbinu ya uandishi yenye kukipa kitu kisicho uhai sifa ya kitu chenye uhai. Kwa hivyo vitu visivyokuwa na uhai hupewa sifa za binadmau. Mbinu hii hutumiwa kusisitiza uhusika, kubainisha maana na kuweza kuchora picha ya kueleweka kwa msomaji au msikilizaji.

Mifano:

(i) Moto ulilimeza jengo. Kumaanisha jengo lote liliteketezwa na moto.

(ii) Majengo mengi yalisimama kwa msongamano.Kumaanisha majengo mengi yalijengwa karibukaribu sana.

(iii)Macho yangu yalishiba picha za wanyama pori . Hapa macho yamepewa uhai kuwa yalikuwa yametosheka kuona picha za wanyama pori.

(iv) Majumba makubwa ya kifahari yaliketi kwa fahari chini ya mti. Majumba ya kifalme yalikuwa chini ya miti kuonyesha tabaka la utajiri na utawala

(v) Miguu yangu ilishindwa kunibeba ilipochoka. Yaani miguu ilishindwa na mwendo.Kwa maoni yetu, mbinu hii ya uandishi huipa hadithi uhai na kumshirikisha msomaji kimawazo.

### 2.2.4 Onomatopeia / Tanakali za sauti

Onomatopeia ni hali ya kutoa mlio amasauti ya jambo ama kitendo kifanyikapo.[T.Y]

Onomatopeia ni mbinu ya uandishi ama usemaji ambapo maneno ya uandishi ama usemaji uhutumika kutoa na kuchora picha ya kuaminika na kumburudisha msomaji au msikilizaji

Mfano

(i) Maji yalidondoka ndo! ndo!ndo!

(ii) Kipande cha jiwe kilianguka majini chubwi!

(iii) Kengele iligogwa nge! nge! nge!

(iv) Fatuma aliteleza topeni prrri! Na kuanguka tapwa.

### 2.2.5 Taharuki

Ni hali ya kuwa na wasiwasi, kutaka kujua ni nini kitakacho jiri.Aidha kabla ya jambo kutendeka au baada ya kisa kutokea.

Hii ni mbinu ambayo msanii huitumia ili kuifanya hadhira kuwa na hali ya kusubiri na kuwa na hamu kutaka kujua kitakachotokea baadaye, na jinsi ya kutokea kwake katika riwaya au matini. Hali hii humfanya msomaji kutaka kusoma zaidi ili kufahamu yatakayo ibuka.

Mifano:

i. Mwalimu mkuu Bwana Pesa, alinita mwendo wa saa sita mchana. Sijui kama nilikuwa nimefanya nini, wakati huu.

ii. Ndivyo alivyofanyiwa waziri huyo…

iii. Nilinyapanyapa kama paka amnyapiavyo panya kisha nikachungulia dirishani na kushangazwa na vioja…

iv. Kwa hivyo tulipita mlangoni kimya kimya. Giza lilishaanza kuingia …

v. Niligeuka na kuanza kutimua mbio kama swara , huku umati wa watu …

### 2.2.6 Urudiaji/ Ukariri

Ni ile hali ya kurudiarudia maneno au sentensi katika mazungumzo au maandishi kwa dhamira fulani. Huu ni ufundi wa urudiaji wa baadhi ya maneno kimakusudi katika matini kama vile riwaya.Mbinu hii hunuwia kusisitiza utendaji,kuakisi utendaji wa matukio,kuyafanya matendo au matukio kuwa bayana .Pia riwaya hueleweka na hutoa hisia fulani ama mawazo kwa hadhira kuhusu kazi waisomayo au wanayoisikiliza.

Mfano

(i) Wanafunzi walicheka na kucheka hadi mabavu zikawauma.

(ii) Fatuma alikimbia akakimbia lakini hakushinda mbio hizo za mita mia moja.

(iii)\Mvua ya masika ilinyesha ikanyesha kwa siku kumi kidindia.

(iv) Kaka Katana alilia na kulia lakini hakupata mtu wa kumfariji.

(v) Nilipiga kelele na kupiga kelele lakini hakuna mtu aliyekuja kuniokoa.

**2.2.7 Methali**

Ni usemi wa busara wa maneno unaokubaliwa na kutumiwa na jamii husika.

Methali ni usemi mfupi wa kisanii ambao ni wa kimapokeo, unaofikiriwa na jamii kuwa kweli. Unatumiwa kufumbia au kupigia mfano na huwa umebeba maana pana kuliko maneno yenyewe yanayotumiwa.Methali hutumiwa kumalizia hadithi ya maadili mema. Methali hutoa ukweli halisi wa matukio katika fasihi. Pia huonyesha mambo yanayopendeza au kufaa. Hutumiwa kutoa muktasari wa hoja na dhana tofautitofauti.

Baadhi ya mifano ya methali ni :

(i) Debe shinda haliachi kutika.

(ii) Mwenda tezi na omo marejeo ni ngamani.

(iii) Haba na haba hujaza kibaba.

(iv) Kikulacho ki nguoni mwako.

(v) Dalili ya mvua ni mawingu.

(vi) Palipo na nia pana njia.

### 2.2.8 Uashiriaji

Huu ni uonyeshaji wa jambo au kitu fulani kwakutumia kitu kimoja kusimamia dhana maalum.

Uashiriaji ni mbinu ambayo msanii huitumia kuonyesha utumiaji wa kitu kimoja kuwakilisha kitu kingine maalum. Kwa mfano gharika inaashiria huzuni au kutokuwa makini. Njiwa kwa kawaida ni kiashiria cha amani.Mifano katika sehemu hii ni:

- **i.** Jeshi la Nzige limeenda mjini-Wanajeshi wengi wameenda mjini.
- **ii.** Ni kipofu wa makosa yake-Yaani mtu huyo haoni makosa yake.
- **iii.** Barabara ilikuwa bahari ya wapita njia-Barabara ilikuwa na wapita njia wengi.

### 2.2.9 Mazungumzo

Haya ni masimulizi juu ya hoja fulani yafanywayo na watu.

Hali hii hutokea pale ambapo kuna mazungumzo baina ya watu wawili au zaidi . Mazungumzo kwa kawaida hupitishwa kwa njia ya usemi taarifa. Mbinu hii hutumika ili kuifanya hadithi ipendeze. Pia huifanya hadithi kuwa hai na kumnasa msomaji au msikilizaji.

Mfano

“Bibi, nimeona nyoka!”

“Wapi ? aliuliza Bi Kadzo akiwa na shaka”.

“Juu ya kitanda chako bibi. Aliniangalia kwa macho “mabaya.”[T.Y]

### 2.2.10 Uchekeshaji

Huu ni utendaji au utumiaji wa neno,maneno au usemi kwa lengo la kuzua ucheshi.

Uchekeshaji unarejelea thamani ya kitu au jambo ambalo huifanya hadithi kutufurahisha na kutuburudisha . Uchekeshaji hutumiwa kuthibitisha wazo au hoja na kuifanya hadithi kupendeza. Msanii huzuwa ucheshi kwa kutumia mchezo wa maneno pamoja na utiaji chumvi katika kazi yake.

Mchezo wa maneno.

Huu ni ujuzi wa uchezeaji wa maneno hasa pale ambapo neno lina maana nyingi. Mbinu hii pia hudhihirika pale ambapo neno linatamkika sawa na jengine.

Kwa mfano

(i) Kiatu cha zamani cha Upele kiko katika mkondo wa mwisho.

(ii) Njiwa ni ndege wa herufi nne.

(iii) Alikuwa akimhifadhia ili amkopeshe pesa.

Hii ni mbinu ambayo msanii huitumia kueleza jambo au kitu kupita kiasi,yaani huenda akatumia yasiyo ya kweli . Lengo kuu la msanii ni kumchekesha msomaji au msikilizaji.Hivyo basi humfanya kuendelea kuisoma au kuisikiliza hadithi kwa makini.

Kwa Mfano

(i) Dada hutumia mamilioni ya pesa kwa siku moja.

(ii) Matano ni kamusi tamba.

(iii) Kama ningekuwa na pesa, ningemjengea mama kasri.

(iv) Tunaishi katika nyumba yenye boma kwa kuwaogopa wezi.

(v) Nyumba hii ni joko hailaliki.

### 2.2.11 Nahau

Ni utumiaji wa maneno mawili au zaidi.Maneno hayo hayawezi kutoa maana ya yale yakusudiwayo kwa kuchunguza neno moja wapo.

Nahau ni makundi ya maneno ambayo maana zake hazitolewi ama hazipatikani kutoka kwa neno moja. Kwa mfano "samaki mkunje angali mbichi" Katka nahau hii hakuna uhusiano wowote na samaki  wala mbichi. Nahau hii ina maana kuwa jambo likitokea basi litatuliwe haraka iwezekanavyo. Kama mtoto ni mtovu wa adabu, basi ni adhibiwe na kuelekezwa katika njia ya sawa.Matumizi ya nahau katika riwaya huboresha kazi ya uandishi na kuonyesha uhalisia wa kipekee.

Mifano

(i) Kwa udi na uvumba-Kwa vyovyote vile.

(ii) Kwa jua na kwa mvua-Kwa hali yoyote ile.

(iii) Kuwa na raha na karaha-Kwa furaha na shida.

(iv) Bega kwa bega-Kushirikiana sawasawa.

(v) Kumvuta mtu mguu -Kumfanya mtu atembee haraka.

### 2.2.12 Kirai Kitenzi

Kirai kitenzi ni fungu la maneno (Kawaida kitenzi kisaidizi na kielezi ama kihusishi) ambapo maana ni tofauti na neno moja binafsi. Usemi huu ukitumika sawa sawa huifanya lugha ya Kiswahili kupendeza na kuwa bora.

Mifano

i.) Kupiga vijembe – kusengenya.

ii.) Kungo'a nanga – Kuanza safari.

iii.) Kumpigia mbuzi ngoma – Kumfanyia jambo mtu ambalo halina faida kwake.

iv.) Kuinua mikono juu – Kufa moyo, kukata tama.

**2.2.13 Sadfa**

Hii ni mbinu ya uandishi. Hali hii hubainika pale ambapo jambo au mambo mawili au zaidi yametendeka kwa wakati mmoja. Matukio hayo huwa hayakupangwa kabisa. Hata hivyo mambo haya huwa na maana katika hadithi au riwaya yenyewe. Vivyo hivyo tumeweza kunena kuwa, mambo yatukiayo kwa wakati mmoja, huwa yana uhusiano katika kazi ya kisanii.

Mifano

(i) Nyamawi alikuwa akienda Mombasa ambako Bozo alikuwa akienda pia.

(ii) Mbodze kupika wali wa nazi, ambapo Tabu rafiki yake alikua anautamani sana.

(iii) Bakari alikwenda ufuoni kuogelea ambako Ramadhani alikuwa akielekea (mf.w)

**2.2.14 Taswira**

Taswira ni mambo au fikra azipatazo msomaji akilini mwake. Fikra hizo huzipata baada ya aidha kusikiliza hadithi au baada ya kuisoma riwaya fulani. (T.Y)

Mbinu hii humshirikisha msikilizaji au msomaji kwa kudadisi mawazo ya wahusika katika hadithi.

**Mifano**

(a) Saumu alikuwa amevaa rinda jeupe na viatu vyeupe pepepe vilivyo mchukua sawasawa.

(b) Tsuma alijenga nyumba yamawe, na kuipaka chokaa, kisha na rangi nyekundu.

(c) Sidi alijuta na kusimama, akashika fimbo na kuanza kumcharaza katana mgongoni hadi chini (mf.w)

### 2.2.15 Balagha

Hii ni mbinu ya kuuliza maswali ambayo hayahitaji majibu ya hapo kwa hapo. Maswali yenyewe hukusudiwa kumfikirisha anayesikiliza au anayesoma riwaya. Lengo hasa ni kumwezesha msomaji au msikilizaji kufikia uamuzi wake mwenyewe juu ya hadithi aisomayo.

Mifano

(i) Mbona maswali yalikuwa magumu?

(ii) Je, amechangia kitu gani katika usomi?

(iii) Na nyinyi mlipataje mali? Mbona mwaringa kama tausi?

### 2.2.16 Njozi

Njozi ni fikra, picha aionayo akilini mtu aotapo. Njozi humwezesha mtu kufahamu mambo yajayo. Pia humwezesha mtu kukumbuka mambo yaliyotendeka mwanzoni.

Mbinu hii humfanya msomaji kuwa na uzungumzinafsia wa ndani kwa ndani kuhusu mhusika au wahusika wa hadithi. Hivyo basi kumhusisha vilivyo katika uwazaji.

**Mfano**

Pili anaota amepita mtihani wake wa taifa darasa la nane. Anaota amepata alama mia nne na sabini. Jina lake latangazwa katika vyombo vya habari redioni, katika runinga na magazetini.

Katika hali ya kweli, pili alikuwa darasa ka nane na alikuwa amefanya mtihani mwaka huo (2012).

Matokeo yalipotangazwa, hakika jina lake lilikuwa midomoni mwa watu. Kwani aliushinda mtihani kwa kupata alama mia nne na hamsini. Kwa hivyo ndoto yake ilikuwa tabirio ya mbambo halisi.

**2.2.17 Barua**

Tuseme kwamba barua ni maandishi yanayoeleza hoja, ujumbe au tukio lolote. Maelezo hayo sharti yafuate kanuni zinazotakikana. Hapa tumesema kuwa, kama ni barua basi, ni lazima mpangilio wa barua ufuatwe.

Mbinu hii hutumika katika kazi za kifasihi. Lengo ni kupitisha habari fulani kwa njia iliyowazi.

Mwandishi hutumia mbinu hii ili kumfanya msomaji kupata ukweli wa mambo wa hadithi.

*Ponda Mali Leo,*<br>*S. L. P. 563,*<br>*Kazole.*<br>*12-10-2014.*

*Kwa Rehema,*<br>*Ni matumaini yangu kuwa u mzima wa afya. Huku kwetu Kazole, sote tu wazima. Tunaendelea vizuri na shughuli zetu za kujenga taifa.*

*Kusudi hasa ya barua hii ni kukujulia hali yako, na pia vile unavyoendelea shuleni.*<br>*Ningekuomba ujibidishe sana masomoni, kwani elimu ni ngao. Itakukinga dhidi ya ufukara siku za usoni.*

*Tuonane wakati wa likizo ya Disemba.*

*Ni mimi nduguyo.*

*Swaga Mali*

Hivyo basi msomaji wa barua huyaelewa mambo yasemwayo kwa njia ya moja kwa moja.

### 2.2.18 Nidaa

Nidaa ni hali ama hisia inayobainika moyoni, inayosababishwa na sauti fulani. Sauti hiyo huenda ikawa ya furaha ama huzuni (T.Y).

Mbinu hii hutumiwa na waandishi ili kuonyesha bayana hisia za wahusika mbalimbali.

Mifano;

Shabashi! __________ Kuonyesha furaha.

Jamani! ____________ Kuonyesha mshangao.

Ondoka! Ondoka haraka! __________Kuonyesha hatari fulani.

Nyanya ameaga dunia! ____________ Kuonyesha huzuni.

Tumeona kuwa mbinu hii humfanya msomaji kuhisi vile wahusika wanavyo hisi. Pia ni mbinu ambayo mwandishi amekusudia kupitisha hisia zake kwa msomaji.

### 2.2.19 Kuchanganya ndimi

Huu ni ujuzi wa mawasiliano, ambapo mzungumzaji hutumia lugha zaidi ya moja (T.Y).

Mbinu hii hutumiwa na waandishi kupitia kwa wahusika wao katika hadithi. Kwa hivyo wahusika wengine hupewa uwezo wa kuzungumza lugha zaidi ya moja. Uwezo huo huweza kuwatofautisha kielimu, kitabaka na hata kimapato.

Mfano:

Zakaria: Mbona Zainabu hunipi salam?

Zainabu: What are you? Mimi huwapa salam rich men.

Mfano huu umeonyesha vile Zainabu anavyojichukulia, amejiweka katika tabaka la juu. Si sawa na Zakaria.

### 2.2.20 Kejeli

Hii ni mbinu ya matumzi ya maneno au usemi ambao utatoa stihizai kwa mtu au mhusika. Kwa ufupi ni njia ya matumizi ya maneno ambayo yanaashiria mzaha kwa mtu ama mhusika. Madhumuni ya kejeli ni kuchekesha, kuburudisha na kuchangamsha hadhira. Kejeli zipo za aina mbili nazo ni kejeli ya maneno na kejeli ya hali.

#### 2.2.20.1 Kejeli ya maneno

Aina hii ya kejeli ndiyo sahili au nyepesi zaidi. Mzungumzaji huzungumza kinyume cha jambo angelipenda kulizungumza.

Mifano

a) Bwana Pondamali alimpiga kijembe Bi Zaituni, kwa kumwambia kwamba ana kiuono cha nyigu-Kumaanisha Zaituni ana kiuno chembamba kama cha nyigu.

b) Fatuma amezaa mtoto wa kiume.

   Fatuma amejifungua mtoto wa kiume (tasfida)

c) Kandawala aliketi juu ya behewa akiendesha treni, badala ya kuwa ndani ya chumba chake maalum, ajabu hiyo.

#### 2.2.20.2 Kejeli ya hali

Kejeli ya hali hutokea wakati mzungumzaji ama mwandishi ameibua mshangao ambao ni kinyume na vile mtu angetazamia. Hali hii itokeapo huibua ucheshi na hutia hofu kwa mhusika kama si kioja.

Mfano

Mwaka wa elfu mbili na mbili (2002), Raila Odinga alisema “Kibaki tosha”. Na kweli alimfanyia kibaki kampeni kwa dhati. Akiwa na matumaini kuwa Kibaki amalizapo kipindi kimoja cha miaka mitano angeng’atuka uongozini. Ilipofika mwaka wa elfu mbili na saba (2007), Kibaki alikitetea tena kiti cha urais (mf.w).

Tumeona kwamba huu ni mfano mzuri wa kejeli ya hali. Raila Odinga alimtendea Kibaki wema kwa kumpigia debe kote nchini, awe rais wa awamu ya tatu. Kinyume chake ni kwamba matarajio yake hayakutimia.

### 2.2.21 Sintaksia

Ni mbinu ya uundaji wa sentensi zilizo na muundo tofauti tofauti. Sentensi zinaweza kuwa fupi ama ndefu. Tumesema kuwa, sintanksia ni mbinu ya uandishi ambayo inajihusisha na upangaji wa sentensi. Upangaji huu sharti ufuate sheria na kanuni, pamoja na uhusiano wa maneno katika hadithi.

Mwandishi huamua kuandika aidha sentensi sahili, ambatani, changamani ama ambatani changamani. Sentensi pia zaweza kuandikwa kuonyesha kinyume.

Mifano

i. Kalamu imepotezwa.

ii. Maisha ni magumu lakini lazima watu waishi.

iii. Zola alijitahidi kwa udi na uvumba kuwasaidia watu wa familia yake, hata hivyo wakati wa kupiga kura alirushwa na watu wake.

iv. Darasa lililojengwa mwaka jana, lilibomolewa na kamati pinzani ya shule.

Kwa maoni yetu, sentensi zikiandikwa sawasawa huwa nyenzo bora kwa mwandishi. Kwani huweza kupitisha ujumbe na kufikisha malengo yake kwa msomaji.

## 2.3 Hitimisho

Kutokana na maelezo, tumeona kuwa waandishi hutumia mbinu mbalimbali kuweza kupitisha mawazo yao kwa hadhira. Mbinu za uandishi ndiyo nyenzo muhimu katika uboreshaji wa kazi za nathari mfano riwaya. Tumeangazia mitindo mbalimbali ambayo baadhi yazo ni tashbihi, sitiari, tashihisi, onomatopia au tanakali sauti, taharuki, urudiaji, methali, mazungumzo, uchekeshaji, nahau, kirai kitenzi, kejeli na kadhalika.

Vivyo hivyo tumejadili kwa ufupi maana ya riwaya. Riwaya ni hadithi ya kubuni yenye vitushi mbalimbali. Iwe na urefu wa kuridhisha. Lazima iwe na mgogoro, wahusika, mandhari na sura. Kwa jumla tumegundua kuwa kuna mbinu nyingi za uandishi. Msanii atumiapo mbinu za uandishi vizuri bila shaka kazi yake itapendwa na wasomaji wengi.Sehemu hii ya mitindo ya riwaya imetufaa, kwani kazi yetu ya utafiti ni mtindo wa *Vipanya vya Maabara*. Katika riwaya hii, tumeamua kujadili baadhi tu ya vipengele vya mtindo ambavyo vimeangaziwa na Mbatia.

## SURA YA TATU

## MTINDO WA VIPANYA VYA MAABARA

### 3.0 Utangulizi

Katika sura hii ya tatu tumejadili kipengele cha mtindo wa usanii. Mtindo unajumuisha mbinu mbalimbali ambazo msanii anaweza kuzitumia ili kulitokeza umbo la kisanii la kazi yake, ili kuwe na athari ya ujumi au uzuri katika kazi hiyo. Mtindo kama kipengele cha fani ni sehemu muhimu ya kazi ya kifasihi. Mtindo kwa jumla unahusiana na namna msanii ametumia lugha kuiumba kazi yake ili iwe ya kuamsha hamu, msisimuko na kuvutia msomaji. Katika mtindo tunajadili baadhi ya vipengele vya *Vipanya vya Maabara*ambavyo vina athari kubwa kwa msomaji. Vipengele hivi ni pamoja na, italiki, tamathali za semi, jinsi mawazo yanavyowasilishwa na sintanksia. Kwa upande wa tamathali ya lugha tunaangazia mbinu kama tashbihi na maswali ya balagha, methali, takriri, nidaa, tasfida, ritifaa na tashihisi na kuchanganya ndimi. Kwa upande wa uwasilishaji wa mawazo tunachunguza aina mbili, nazo niuwasilishaji halisi huru wa mawazo na uwasilishaji halisi wa mawazo.

### 3.1 Dhana ya Mtindo

Dhana ya mtindo inarejelea namna msanii wa kazi ya kifasihi anavyojieleza. Kulingana na Frye na wenzake (1985:447) mtindo unarejelea jinsi msanii anavyotumia lugha kujieleza. Hivi ni kusema kuwa mtindo unahusiana na jinsi msanii anavyoijenga matini ya kifasihi kwa kutumia lugha kwa sababu ya kubuni umbo la kisanii linalopendeza na kuvutia. Kwa mujibu wa Holman (1976:320) mtindo una vitengo viwili, jinsi wazo linavyodokezwa na ubinafsi wa mwandishi. Kwa hivyo, mtindo hulenga kudhihirisha

ubinafsi wa mwandishi, mawazo na lengo la fikra zake. Kwa kauli hii mtindo unaweza kurejelewa kama mtu au usanii wa kazi husika. Kwa hali hiyo, tunaweza kuwa na mtindo–mtu na mtindo–usanii. Mtindo–mtu ni aina ya mtindo unaotumiwa na mwandishi mmoja kumtofautisha na waandishi wengine wa kazi ya kifasihi.

Wamitila (2003:145) anadai kuwa kazi za Mohamed Said Ahmed zina matumizi mapana ya jazanda na sitiari pamoja na unyumbufu wa kisintaksia tofauti na kazi za Adam Shafi zilizo na lugha nyepesi na uchache wa tamathali. Hivyo basi tunaweza kuwatofautisha waandishi hawa kwa mitindo yao. Kwa upande mwingine mtindo–usanii ni aina ya mtindo unaofungamana na muktadha wa kazi yenyewe na hali zinazojitokeza katika kazi hiyo. Katika uhakiki huu tumerejelea mtindo–usanii kwa kuangalia riwaya hii kwa upekee wake.

Mbali na hayo, mtindo kama wanavyosema akina Frye, unaweza kuwa ni kipindi maalumu cha wakati. Huu basi unaweza kuitwa mtindo kipindi kwa kurejelea kipindi maalumu na muhimu cha wakati wa kihistoria. Wakati wa kipindi kama hicho huweza kuzuka mtindo wa namna kazi za kifasihi zinavyoandikwa. Kwa mfano, katika kipindi cha mwongo mmoja uliopita baadhi ya riwaya za Kiswahili zilizoandikwa zina mwelekeo mkubwa wa kutumia mbinu za mtindo wa riwaya mpya. Mbinu ambzo riwaya hizi zimetumia ni kama vile lugha ya kitamathali, sintaksia yenye pengo, uzungumzinafsia, uhalisiajabu, uwasilishaji wa mawazo kisaikolojia, mbinu za kibalagha na italiki. Mifano ya riwaya hizi ni *Bina–Adamu!, Musaleo!, DuniaYao na Babu Alipofufuka*. Mtindo unaojibainisha katika kazi hizi unaonyesha mtindo–kipindi wa mwongo tuliotaja. Mtindo

kama kipengele muhimu cha fani hutumiwa kukuza na kuendeleza maudhui pamoja na dhamira katika kazi za kifasihi. Mtindo hutekeleza haya kwa kutumia mbinu mathalani usimulizi, uwasilishaji wa mawazo na lugha ya kitamathali miongoni mwa mbinu nyingine.

Kwa mujibu wa Njogu na Chimerah (1999:47) mtindo ni nyenzo kuu ya kusanifu kazi nzima. Hii inamaanisha kuwa mtindo ndicho kipengele kinacholeta ujumi katika kazi yoyote ya kifasihi. Hali hii ndiyo inayoiwezesha matini ya kifasihi kuwa ya kusisimua na kumvutia msomaji.

Uhakiki wa mtindo hujikita katika mbinu za kujieleza kilugha ambazo kwazo mwandishi amezitumia kwenye kazi yake. Henderson na Wenzake (1994:9) wanadai kuwa uhakiki huu hujihusisha na uteuzi wa muundo wa sentensi, msamiati na mbinu za kitamathali mfano sitiari, tashbihi, taashira na ishara zinazobainisha toni na kuonyesha ubinafsi wa mwandishi. Kwa maoni yetu tumesema kwamba hivi sivyo vipengele pekee vya kuhakikiwa katika mtindo. Kunavipengele vingine kama usimulizi, mtazamo, uwasilishaji wa mawazo, uchimuzi, muwala na mshikamano, lugha na itikadi. Kunazo pia mbinu nyingine za kitamathali kama tasfida, matumizi ya maswali ya balagha, kinaya, usambamba, dhihaka, tashtiti, chuku na takriri. Vile vile mtindo unaweza kuangaliwa kama nyenzo ya kuvijenga vipengele vya fani mathalani uhusika na wahusika pamoja na ploti. Kwa kutoa mfano, kuna mtindo wa kujenga ploti kwa kutumia mbinu elekezi, mbinu rejeshi, uzungumzinafsi ndani na mkondo wa ung’amuzi.

Mtindo wa usawiri wa wahusika unaweza kuchanganya pamoja  na usawiri wa wahusika kisaikolojia, kiishara, kisitiari na ukuzaji wa wahusika changamano au sahili. Katika uhakiki huu tumevichunguza baadhi ya vile vipengele vya mtindo ambavyo huenda vikawa vina athari kwa msomaji katika matumizi yake kwenye riwaya husika. Hii ndiyo maana, iliyotupelekea kuamua kuhakiki- sintanksia, tamathali za lugha, italiki na jinsi mawazo yanavyowasilishwa katika *Vipanya vya Maabara.* Aidha katika uhakiki wowote ule mhakiki hawezi kuhakiki masuala yote kwani anadhibitiwa na muda uliowekwa, upeo na mipaka wa kazi yake.

### 3.1.1 Sintaksia ya Mapengo (Dukuduku)

Hii ina husu muundo wa sentensi. Hapa tumeangalia jinsi nukta na kistari vilivyotumika kuwa sawa na sentensi ilivyo na mapengo.

Kulingana na Frye (k.h.j. uk.446), riwaya ambayo hasa ni ya kisaikolojia hubainisha wingi wa mawazo kupitia sintaksia yenye mapengo, sentensi zisizokamilika, herufi kubwa, matumizi ya mistari, dondoo, wino mzito, sentensi zisizoakifishwa na italiki. Hizi ni mbinu ambazo ni muhimu katika upimaji wa mawazo ya wahusika na athari kwa wasomaji wa matini husika. Japo kazi yetu haihusu mambo ya kisaikolojia, lakini mawazo haya yametusadia sana kujua baadhi ya vipengele vya kimtindo.

Sintaksia ya mapengo ni istilahi ambayo tumetumia kurejelea mpangilio au ujenzi wa sentensi ulio na nafasi wazi. Nafasi hizo wazi huwa zina nukta au kistari kifupi kuchukua nafasi ya maneno ambayo yamemalizia kuunda na kukamilisha sentensi.

Matumizi ya nukta na kistari kifupi huonyesha udondokaji wa fikra za wahusika. Kwa kauli nyingine tumeweza kusema kwamba matumizi ya mbinu hizi hubainisha jinsi mawazo ya mwanadamu yalivyo katika ung'amuzibwete na yanapodokezwa basi huacha nafasi zilizo wazi ambazo zinafaa zijazwe kwa kupangwa upya ili sentensi hizi au mawazo yawe na mshikamano wa kimantiki.

Kwa mintarafu hii basi, utumiaji wa nukta na kistari huweka wazi uhalisia wa mawazo ya binadamu yalivyo na hata pia uchangamano wa mawazo yenyewe. Nukta na kistari vikitumiwa katika matini husika huana athari kubwa kwa msomaji .Kwani humfanya atafakari kinachosemwa ili aweze kubaini maana inayokusudiwa kama inavyojibainisha katika sentensi hii. *Nilienda kupekuapekua ndani ya pochi, nikatoa kalamu, picha ndogo ya mwanamke wa kizungu – labda mwenye pochi – na noti za dola mia moja* (uk. 170).

Hapa Bob anaendelea kuikagua pochi iliyokuwa ya mwanamke huyo wa kizungu aliyeuliwa na waziri Rashid. Hivyo basi katika sentensi hasa kwenye kistari ama vistari inaonyesha kuna maneno ambayo yameachwa ili msomaji ajijazie. Kwa mfano, tunajiuliza mwanamke wa kizungu kutoka Uingereza ama ni mwanamke wa kizungu aliye na uraia wa Amerika? Pia msomaji anaweza kujiuliza, je mwenye pochi mlikuwa na dola tu za kimarekani mia moja?

Mfano mwingine: "*Hao? Adimu kama…. Wanasemaje vile*?" (uk. 39). Hapa Bob anajifanya kushangaa kwa kutowaona wazazi wa Wairi katika sherehe ya binti yao ya kuadhimisha siku ya kuzaliwa. Katika sentensi aliyosema Bob, kuna alama za nukta

zilizowekwa, kuonyesha kwamba kuna neno au maneno msomaji akamilishe, pengine kabla ya yule anayezumgumza na Bob–Wairi kukamilisha. Hapa msomaji sharti afahamu kwamba kauli hiyo ni tashbihi. Hivyo basi atasema kuwa pengine wali wa daku au kaburi la baniani. Mbinu hii inazidi kumhusisha msomaji katika kufikiri na kuchangia katika mawazo ya msanii.

Tumeona kwamba mbinu ya nukta na kistari imetumika sana katika *Vipanya vya Maabara*. Baadhi ya mifano inapatikana kurasa za 79, 91, 83, 99, 106, 130, 133, 134, 143 na katika kurasa nyingine katika riwaya hii.

Matumizi ya herufi kubwa pia yamebainika katika riwaya hii. Kama tulivyotangulia kusema kwamba mbinu hii ni muhimu sana katika uakisi wa mawazo ya wahusika na pia athari kwa saikolojia ya msomaji katika *Vipanya vya Maabara*. Herufi kubwa zimeweza kutumiwa na mwandishi kwa lengo la kumteka msomaji hisia zake na kuweza kudadisi yasemwayo na wahusika. Baadhi ya mifano iliyotumika ni. SI RUKSA KUINGIA BILA KIBALI CHA MPOKEZI (uk.14). ORIGINAL, REPUBLIC OF KENYA: TEMPORARY PERMIT, OCCUPATION, BUSINESSMAN, PASSPORT CONTROL OFFICE – NAIROBI, KENYA (uk.121).

HIFADHI ZA ZIWA MANYARA

LAKE MANYARA NATIONAL PARK (uk.153)

“SENETA WA MAREKANI AINGIA NCHINI KUMTAFUTA MWANAWE” (Uk. 177).

Mbali na baadhi ya maneno na sentensi kuandikwa kwa herufi kubwa, tumeona pia sura za riwaya zimeandikwa kwa mfumo huo huo wa herful kubwa. Dhamira zaidi ya mwandishi kufanya hivi, ni aweze kummakinisha msomaji na kuyafumbata yanayoendelea katika hadithi anayoisoma.

### 3.1.2 Italiki

Kulingana na Mathews (1997:189) italiki inatumiwa kusisitiza na kuonyesha maneno pamoja na mifano ya dhana na maoni katika maandishi. Kwa kawaida italiki huandikwa kwa mwandiko wa mlazo kuelekea kulia. Kwa upande wa fasihi, kama anavyogusia Shaw (1972:208), italiki inatumiwa ili kutofautisha mawazo, maneno na dhana tofauti tofauti ili kuweka msisitizo kwa msomaji. Kusudi la utiaji mkazo, hutekelezwa ili msomaji ayape maandishi ayasomayo umakini na kuyatazama kwa jicho pevu. Kwani mkondo huu unaathiri utafakaraji wa msomaji kwa kumwezesha amakinike, hivyo basikuathiri saikolojia yake katika ung'amuzi na uwezo wa bongo lake. Kwa mintarafu hii tumeweza kusema italiki pengine hutumiwa barabara katika upimaji wa saikolojia ya msomaji.

Katika uhakiki wetu wa *Vipanya vya Maabara*, tumegundua italiki imetumika kurejelea anwani, vitu, maandishi kutoka nakala zingine, maneno ya lugha nyingine, barua na hata maneno yaliyotamkwa na wahusika. Waaidha, italiki inapotumika kubainisha maneno na barua na mambo mengine huyafanya yatiliwe maanani na msomaji na kwa hivyo kusisitiza kushirikiana kwake na ujumbe anaousoma. Mifano ya matumizi ya italiki ni kama ifuatayo.

Vitu: *Pesa (Uk. 11)*
Anwani ya kitabu*: Uhuru wa watumwa (Uk. 11)*
Maneno: *Wambuyu, Matinii (Uk. 34)*
*Darling (Uk. 16)*
*Birthday, serious, cheers (Uk. 35)*
*Dignity (Uk.78)*
*Black American (Uk.91)*
*Buffet (Uk.127)*

Maneno katika italiki yametumiwa kuleta msisitizo, mnato na nguvu maalum kwa msomaji. Mwandishi ametumia maneno ya kawaida kusisitiza ujumbe ujitokeze kwa nguvu na kuwa mguso kwa msomaji.

Italiki vile vile huweza kuakisi usemi mahususi wa mhusika au wahusika kama inavyojibainisha katika kauli hii ya uzungumzinafsia wa Bob alipokuwa ameenda kumzuru Wairi kumjulia hali yake kule ilimokuwa *Rafiki Massage Parlour*.

*Ukimwi utatawala kizazi hiki mpaka lini*? (Uk. 191)

Bob hapa anaulaumu ukimwi kwa kuwaua vijana na inaelekea kwamba, wakati umefika kwa wataalam wa tiba kuweza kuvumbua tiba–vijana wamechoshwa.

*Hapana! Wairi hatakufa,…* (Uk. 192)

Katika usemi huu Bob anajipamoyo kuwa rafiki yake Wairi hatakufa kamwe kutokana na gonjwa la ukimwi. Hata hivyo mbali na kauli hizi kuakisi yaliyosemwa na mhusika huyu, italiki na maswali ya balagha, yanamwongoza msomaji-katika tafakuri ya mhusika ili kumtambua Bob na yale yanayomkumba moyoni na akilini.

Usemi mwingine ambao umeandikwa kwa italiki ni *sijinyime utamanicho* (Uk. 157). Maneno sijinyime utamanicho yalikuwa yameandikwa katika kipande cha leso, cha Rehema, mtaalishi. Leso hiyo ilitandikwa juu ya mwamba ili wote watatu yaani Vera – mwanamke wa kizungu, Bob na Rehema mtaalishi walie chakula. Maneno haya yalizidi kumuumiza Bob hisia zake za kimapenzi kwa Vera. Kwa kuwa Vera alivua nguo zake, viatu na akabaki na chupi peke yake. Hakua na sidiria. Kisha akapanda juu ya mwamba mkubwa zaidi na kumuomba Bob ampige picha. Hivyo basi usemi huu kwa vile ulivyoandikwa humfanya msomaji kuvutiwa zaidi na hata kubashiri yatakayojiri mbeleni.

Kuzidi kuonyesha yaliyosemwa hasa na wahusika mwandishi ametumia, pia italiki katika kudondoa habari kutoka gazetini. Hali hii inajidhihirisha hivi.

**‘Nyumba za ukandaji kumbe ni madanguro?”**

> *Gazeti hili limegundua kwamba nyumba za ukandaji jijini humu ni madanguro. Uvumbuzi huo ulifanywa na waandishi wa habari ambao waliitembelea Rafiki Massage Parlour, ambayo ni nyumba maarufu ya ukandaji katika eneo la River Road.*
> *Walijifanya wateja, wakalipa jumla ya shilingi elfu mbili, kila mmoja akapewa mkandaji wa kike. Walipoingia kwenye vyumba vya kukandiwa, waliulizwa kama walitaka huduma za kukandwa au za kufanya mapenzi. Waliambiwa kwamba kama walitaka kufanya mapenzi lazima wangeongeza shilingi mia tano kila mmoja, na wawape fedha hizo wanawake wenyewe badala ya kulipa kwenye mapokezi, ambapo walikuwa wemelipa ada ya elfu mbili. Mmoja wa waandishi wa habari alilipa fedha hizo ili kupata ukweli kamili.*
> *Mwanamke aliyefuatana naye alipoanza kuvua nguo, mwandishi huyo wa habari alimwambia kuwa hakutaka kufanya mapenzi ila alitaka kupata habari fulani kuhusu shughuli za nyumba hiyo. Alifahamishwa kuwa shughuli muhimu pale ilikuwa ukahaba wala sio ukandaji. Alipewa majina ya wanawake watatu, wafanyikazi wa pale, ambao walikuwa makahaba tu. Alielezwa kuwa hali ilikuwa hiyo hiyo katika nyumba nyingine za ukandaji kote jijini.[ Uk. 14-15]*

Makala haya ingawa yameandikwa kutoka gazetini yanadokeza ukweli wa shughuli za uozo wa maadili zinazoendeshwa katika majengo mengi ya ukandaji jijini na hata miji mikubwa kote nchini. Hali hii pia inadhihirisha ukweli kuwa jamii imekumbwa na balaa tumbi tele. Kwa ukosefu wa ajira uliotokana na sera mbovu za serikali. Vijana wengi hasa wa jiji la Nairobi na pengine miji mingine hawana matumaini na kwa hivyo wanajitumbukiza katika ukahaba na ulevi ambao wanadhani utawawezesha kupata mapato ili wasahau shida zao lakini si suluhisho. Hivyo basi makala haya ya gazeti yalioandikwa kwa italiki yanateka msomaji fikira zake na kuweza kuzingatia vizuri ayasomayo na kupima uzito wa habari hizo na athari zake katika maisha ya binadamu wa leo.

Barua (Uk. 160 – 161)

Mpenzi Bob,

> *Nimeona siwezi kusubiri tuonane mwezi ujao wakati wa likizo yangu. Lazima nikueleze mambo yaliyonikaa moyoni. Nakukosa sana mpenzi. Bado nakumbuka siku ya mwisho tulipokutana Nairobi. Tulivyoogelea kwenye furaha ule usiku wa Salama Guest House.*
>
> *Nawaonea kijicho akina Gaceri na Vera, ambao wako karibu nawe kuliko mimi. Labda nilishakuwa kamba ya mbali ambayo haifungi kuni. Najua kwamba unanipenda na kwamba unakutana nao kwa uhitaji tu. Lakini tahadhari na gonjwa la ukimwi. Vijana wanasema ukimwi ndilo jaribio kuu la kizazi hiki. Mimi naamini kwamba utafika wakati ambapo utakuwa tayari kuishi kama mke na mume. Hiyo ndiyo ndoto yangu. Kuhusu habari za chuoni hapa, ni ninaendelea vizuri na masomo yangu. Uchungu wa kunyimwa nafasi ya kwenda kufanya uhandisi katika chuo kikuu cha Nairobi ndio sasa unanitoka. Ile bodi ya kuchagua wanafunzi wa kujiunga na vyuo vikuu mbali mbali ilinitendea dhuluma kubwa. Lakini hayo sasa yamepita. Mpango wangu ni kwamba baada ya kupata BSc katika Chuo hiki, nitaweza kufanya diploma ya kompyuta huko Nairobi.*

*Tatizo langu wakati huu ni mwalimu wangu wa hisabati. Amenisumbua sana kwa kutaka kufanya mapenzi na mimi. Nishamwambia haiwezekani lakini bado ananifuatafuata. Amezoea vibaya. Kufanyia mapenzi na baadhi ya wanafunzi wanaolemewa na somo lake na kuwapitisha kwa kuwapa alama wasizostahili. Lakini mimi sihitaji maksi za bure. Naongoza darasani mwangu katika somo hili. Ngoja tu akiendelea na upuzi wake nitamchukulia hatua – hataamini.*
*Nakomea hapa. Tutaonana mwezi ujao na kuzungumza zaidi. Nisalimie shoga zangu Freda na Wairi, na akina Okach, Swaleh na Muli.*

*Wako wa moyoni,*
*Jamila Ramadhani.*

Barua ambayo imepigwa chapa kiitaliki ni ya mhusika Jamila akimwandikia mpenzi wake wakiume Bob. Jamila ameweza kumtahadharisha Bob juu ya matembezi yake pamoja na akina Vera – mwanamke tajiri wa kizungu na rafikie wa zamani Gaceri. Kuwa Bob asipojihadhari huenda akapatwa na gonjwa hatari la ukimwi. Pia Jamila anaonyesha hakupendezewa kwa kukosa kufanya kozi ya uhandisi chuoni Nairobi, hata hivyo alijitia matumaini kuwa atafanya diploma ya kompyuta punde tu apatapo digrii ya BSc. Vile vile amezidi kumweleza mpenziwe juu ya mwenendo mbaya wa mwalimu wake wa hisabati, kwamba asipogeuza mwenendo atamchukulia hatua.

Kupitia barua ya Jamila, mwandishi amependa msomaji aweze kuzingatia sana yaliyoandikwa na kuweza kuyafuatilia sawasawa. Vivyo hivyo barua imepitisha ujumbe kuwa sio vijana wote wana maadili mabaya. Tumeona jinsi vile Jamila amejali maisha yake na hata ya mpenzi wake kwa kumkumbusha juu ya ukimwi. Kwa vile mhusika Jamila si mtovu wa adabu, ameonyesha wazi kuwa hapendi tabia ya ukahaba kwa kumkatalia mwalimu matakwa yake huko chuoni–kilimo.

Kupitia kwa barua hii, imemuonyesha msomaji, kuwa ufisadi uko nchini katika asasi mbali mbali za serikali na za kibinafsi. Jamila hakusomea uhandisi kwa kubadilishiwa kozi na JAB. Tumejifunza kupitia kwa mawazo ya mhusika kuwa kufanikiwa maishani kwa hitaji bidii na kujitolea kwa dhati. Vile vile siasa mbaya na sera mbovu za serikali hazifai na zapaswa zirekebishwe na viongozi husika.

### 3.1.3 Tamathali za Semi

Wamitila (k.h.j.) anasema tamathali ni neno au kifungu ambacho kina maana iliyofichwa. Ameendelea kusema kuwa matumizi ya tamathali za usemi yamezoeleka sana sio tu katika riwaya ya kazi za kifasihi bali pia katika lugha ya kawaida. Tamathali za usemi zina mchango mkubwa katika kuifanya kazi ivutie, iwe na msisitizo na mnato mkubwa. Baadhi ya tamathali za usemi ni tashbihi, sitiari, tasfida, tashihisi, chuku, kinaya, dhihaka, maswali ya balagha, tabaini na nyingine nyingi.

Tukimrejelea Wamitila (2008:407) anazipanga tamathali za usemi katika makundi manne. Makundi haya ni tamathali za sentensi, tamathali za maneno, tamathali za kisauti na pia tamathali za kitafkiri. Kwa maoni yake tamathali za kisentensi ni pamoja na mdokezo, maswali ya balagha na usambamba. Nazo tamathali za kitafkiria zina jumuisha kijembe, ritifaa, dhihaka na tanakuzi. Tamathali za kisauti zinajumuisha tanakali za sauti, vikae, anafora na tauria. Nazo tamathali za kimaeneo zikichukuwa chuku, tasfida na tabaini.

Kwa mjibu wa Holman (1976:224) lugha ya kitamathali ni kama lugha inayoenda kinyume na kaida za kawaida za uundaji, upangaji na utumiaji wa lugha ili kuleta athari

iliyo mpya na maana. Linalojibainisha ni kuwa lugha hii ni ukiushi wa sheria zilizozoeleka katika mizani ya maana na mpangilio wa maneno katika matumizi ya maana husika. Kwa maoni yetu tumeona kuwa ukiushi huu huwa ni wa kimakusudi na umedhamiriwa kuleta maana mpya na kuzidi kusisitiza ujumbe unaosemwa.

Tamathali huzua na kuchora picha anuwai katika akili za msomaji ambazo kwazo huchangia katika uelewa wa kazi za kinathari na kuacha athari ya kipindi kirefu. Taswira hizi zinazojitokeza kutokana na matumizi mazuri ya tamathali za lugha, ni sehemu ya picha anazoziona msanii katika fikra zake.

Mlokozi (1989:45) anasema kuwa tamathali za usemi ni tungo au kauli fupi za kisanaa zenye kubeba maana au mafunzo ya jamii. Amezidi kusema kuwa tungo hizi hujaribu kuchora picha kwenye akili ya msomaji ili kumwezesha kuelewa ujumbe kwa urahisi na kufuma hisia zake. Hali hii hutokea na huweza kubeba maneno machache lakini yakaweza kutoa maana iliyo na upana mkubwa.

Kwa mujibu wa Mbatia (2001:77) tamathali za usemi ni ukiushi wa kimaksudi wa mtunzi wa lugha katika viwango vya maana (Semantiki)  na mpangilio wa maneno (Sintaksia) ili kuleta maana mpya au msisitizo.

Kwa hivyo tumeweza kusema tamathali za usemi ni maneno, nahau au semi ambazo hutumiwa na waandishi wa kazi za kifasihi ili kuzidi kutia msisitizo katika maana.

Tamathali za semi huleta maana na hupamba kazi ya kifasihi kwa kuongezea na kuboresha utamu wa lugha. Aidha tumeweza kusema kuwa tumekubaliana na Mbatia kwa kuwa katika riwaya yake ya *Vipanya vya Maabara* ameweza kutumia tamathali nyingi za semi zinazoendeleza kuifanya kazi yake kuwa nzuri sana.

**3.1.3.1 Maswali ya balagha**

Kulingana na Wamitila (2003:27) balagha ni dhana inayoelezea sanaa ya usemaji na mbinu za uwasilishaji wa semi kwa njia ya kushawishi na kuathiri msikilizaji. Hivyo basi balagha ni ufundi wa kisanaa wa usemaji, ni uandikaji wenye lengo la kuwasilisha ujumbe kwa msikilizaji au msomaji kwa njia ya kushawishi. Njia hii inalengo la kumfanya msikilizaji au msomaji avutiwe na yanayosemwa au anayosoma.

Kwa upande wake (Wamitila) amesema kuwa maswali ya balagha ni mbinu ya kitamathali ambapo msemaji huuliza maswali ambayo hayahitaji kujibiwa kwa vile majibu yake yako wazi kwa kila mtu. Hii ni mbinu moja kuu ya kusisitiza usemi katika kazi ya kifasihi.

Holman (k.h.j 452) anasema kuwa mbinu hii hulenga kumshawishi msikilizaji kwa kumpa changamoto ya kuyatafuta majibu ili asiwe msikilizaji tuli bali awe mshirika katika mchakato wote wa mawasiliano. Tuseme kwamba balagha ni umilisi na utumiaji

wa lugha kwa njia ya kufurahisha. Hivyo basi tumeona kuwa hali hii humtia msikilizaji au msomaji wa kazi za nathari za Kiswahili ambazo ni fasihi, hamasa ya kuchangamka anayoambiwa au anayoyasoma kwa makini sana.

Mfano wa maswali ya balagha katika *Vipanya vya Maabara*ni wakati Konstebo Kerogo anapoona kuwa jina lake halikusomwa na afisa mkuu wa kituo cha polisi cha Bondeni.

Wakati maafisa wenzake wachanga katika kazi ya polisi wamepandishwa vyeo. Akiwa mlevi nyumbani kwake usiku anasema hivi;

> *…cheeo?....kula cheo?...kazi yap o-poliisi nayo ni kazi? Anaaijali nani nchi hii? (uk. 30)*

Maswali haya yanatupa msukumo wa kuyarejelea maneno yasemwayo na Konstebo Kerogo japo ni mlevi, ili tupate maana kamili. Pia maswali haya yanatufanya kumakinika wakati tunaendelea kusoma matini kwa nia ya kupata ujumbe unaojitokeza katika habari, na kutufanya washiriki wa usemi wake.

Maswali ya balagha pia ni nyenzo ya kuyataja mawazo na hisia za wahusika. Kwa mintarafu hii tunaweza kuingizwa katika mkururo wa uwazaji wa wahusika na kuhisi wanavyohisi. Hivyo basi kwa njia hii tunaweza kuwaonea huruma na kukerwa na dhuluma zinazoendelezwa dhidi yao. Ama tunaweza tufurahie mafanikio yao. Mawazo haya yanajitokeza vizuri pale Bob anapomskitikia babake kwa kutopandishwa madaraka kazini. Bob anasema hivi:

> *Kwa nini mtu anyimwe haki yake kwa kusema ukweli? Mbona tunahimizwa kusema ukweli kila mara kanisani, shuleni na hata*

*hapa nyumbani? Tuseme sasa ukweli umegeuka kuwa kitu kibaya kinachoweza kumletea mtu adhabu? (uk 28).*

Maswali haya yamelenga kutufanya tuathirike na vitendo ambavyo Kerogo babake Bob anafanyiwa na wakubwa wake katika kituo cha polisi cha Bondeni. Katika kifungu hiki cha maswali ya balagha, mwandishi inaonekana alikusudia tuchukue msimamo wa kuona vile Kerogo anavyodhulumiwa kazini. Athari iliyopo ni kwamba vitendo viovu kama dhuluma, ukabila na hongo kazini havifai kamwe na tunapaswa tujirekebishe.

Mwandishi wa *Vipanya vya Maabara* ameweza kutumia mbinu hii ya maswali ya balagha kwa wingi.

#### 3.1.3.2 Tashbihi

Kwa mjibu wa Mohammed (1990:23) anaeleza kuwa tashbihi lazima iundwe kwa misingi inayokubalika kimantiki hasa kulingana na jamii.

Msokile (1993:54) anaeleza kuwa aina hii ya tamathali hutumia mlinganisho wa mambo ama vitu kwa kutumia viunganishi kama, mfano wa, *sawa na,mithili ya,fanana na.* Vitu vinavyolinganishwa mara nyingi huwa ni viwili au zaidi vyenye sifa tofauti.

Wamitila (2003) anasema tashbihi ni ulinganishi wa moja kwa moja. Ulinganishi huu unadhamiriwa kusisitiza sifa fulani na pia kutujengea picha ya aina fulani akilini. Ulinganishi huu unaonyeshwa kwa matumizi ya viungo: kama, mfano wa, sawa na, kama vile, mithili ya, nakadhalika.

Tuki (2004: 398) wanasema kuwa tashbihi ni usemi wa ufananisho au mlinganisho wa vitu viwili au zaidi. Vitu vinavyolinganishwa pamoja ni sharti viwe na ulinganifu wa sifa, umbo, tabia au sura. Sifa hizi ndizo ambazo zinasafirishwa kutoka kitu kimoja hadi kingine.

Katika V*ipanya vya Maabara* kuna tashbihi nyingi ambazo kwazo mwandishi amezitumia ili aweze kupitisha na kujenga picha ya aina fulani kwa msomaji. Hizi hapa baadhi ya tashbihi zinazotumika katika riwaya hii.

*Gari linang'ara kama kioo (UK. 3).*

Hapa Bob amemaliza kuliosha gari la Vera na sasa anamwambia aende nje (kutoka hotelini) akalione na kwamba Bob amefanya kazi yake vizuri. Tunapata picha ya vile gari lilivyo safi na kuwa na mng'ao wa kioo kilicho, bila shaka safi daima.

*Miguu yangu ilitekenywa na zulia laini kama manyoya* (Uk. 79). Zulia ni tandiko gumu lililonakishiwa na ambalo hutandazwa sakafuni. Mazulia ni ya aina au muundo tofauti na bei tofauti. Bob ameingia nyumbani mwa Vera, hivyo basi ni ajabu kwake kwani miguu yake ililambwalambwa na manyoya ya zulia laini. Hapa labda mwandishi anataka kutuchorea picha ya nafasi aliyonayo Vera. Bila shaka zulia hilo ni la bei ghali liwezalo kununuliwa na tabaka la juu wala si tabaka la china kama akina Bob. Tashbihi nyingine inatokana na usemi ufuatao. *Kisha nikavua viatu na kutoa zile soksi chafu zilizonuka kama mto Nairobi* (uk. 135).

Bob ametoka safari Tanzania, amefika nyumbani kuhudhuria hafla ya kufuzu kwa dadake Freda kuwa mtawa na muuguzi. Kwa kuwa amepata hela kidogo na hakuwa na wasaa wakubadilisha nguo, kwani nyumba ilifungwa na funguo zilikuwa na mamake hospitalini Kenyatta. Aliamuru kununua soksi mpya na kuzitupa za kitambo zilizokuwa na uvundo. Tashbihi hii inatoa athari kwa msomaji kwamba soksi za Bob zinanuka sana na zinakuwa hazifai kuwa nyayoni mwake. Sawa na mto Nairobi ambao maji yake yamegeuka uji mzito wa uchafu unukao uvundo.

*Habari hizo ziliniangukia kama mwamba kutoka mbinguni* (Uk. 207). Hapa ni wakati Bob amenunua gazeti na kuona kichwa kidogo cha habari na kusoma maelezo yake harakaharaka. Rafiki yake Swaleh Fadhili alipigwa risasi siku iliyotangulia kwa kuwa ni jambazi.

Hivyo basi tashbihi hii inaathari kubwa kwa msomaji wa matini husika. Inatuonyesha vile Bob anavyohusika sana na Swaleh Fadhili. Kwamba msiba huo ulimuumiza sana moyoni. Kweli mwamba kutoka mbinguni unapomwangukia mtu hawezi kuwa hai. Ndivyo ilivyo na kifo cha Swaleh kwa Bob. Kilimchoma sana. Kwa maoni yetu, tumeona mwandishi ametumia tashbihi hii ili tuone ukuruba uliopo baina ya vijana hawa wawili. Hivyo basi katika uchunguzi wetu tumeona kwamba mwandishi ametumia tashbihi nyingi katika kazi yake. Na karibu zote zinakiunganishi “kama”.
Mbinu hii hutumiwa kuchora taswira au picha ya kitu au mtu kwa njia ya ulinganishi. Sababu ni kwamba ujumbe uweze kueleweka haraka na hadhira ilengwayo na mwandishi.

Kwa maoni yetu tumeona kuwa tashbihi lazima kwanza ikubaliwe na jamii ambao ni watumizi wa lugha. Tashbihi iwe na lengo la kufunza, kuonya na kutahadharisha jamii. Vivyo hivyo, tashbihi sharti iwe na kiunganishi kinachofananisha kitu, dhana au wazo na aidha kitu au kiumbe mwingine.

**3.1.3.3 Takriri**

Kwa mujibu wa Msokile (k.h.j uk. 61) anasema kuwa takriri ni urudiaji wa silabi, maneno, mistari au vifungu vinavyolingana katika kazi za kifasihi.  Kulingana na Ruo Kimani (1982) anaeleza takriri kama urudiaji wa maneno ama silabi kwa madhumuni maalum.

Mbatia (2001) anadai kuwa takriri ni mbinu ya utunzi inayohusu urudiaji wa sauti, neno au mistari fulani.

Ngure (2003) anaeleza takriri kama urudiaji wa silabi au sauti zilizolingana katika maneno yanayokaribiana kimatamshi. Amezidi kusema kuwa wakati mwingine maneno yanaweza kubadilika. Kwa usemi huu, tumesema kuwa takriri ni hali ya kurudia neno au maneno, sentensi, kifungu cha maneno katika matini na vina katika mashairi.

Takriri hujibainisha hasa kupitia marudio ya neno, sauti au hata kwa maneno yale yale ili kutia mkazo zaidi juu ya dhana asemayo mwandishi. Dhamira hasa ya kutumia takriri ni kumfanya anayesikiza au anayesoma matini fulani aelewe umuhimu ulio katika jambo linalokaririwa ama linalorudiwarudiwa.Mtunzi wa *Vipanya vya Maabara*ametumia mbinu hii ya takriri kusisitiza ujumbe unaotolewa na wahusika aliowaumba. Mfano mzuri ni huu ufuatao:

*Furaha tele kwako-oo*
*Furaha tele kwako Wairi*
*Furaha tele kwako-oo*
*Siku hii ya leo-oo*
*Ya kuzaliwa kwako*
*Furaha tele kwako-oo (uk 38)*

Huu ni wimbo alioimbiwa Wairi na rafiki zake wakati wa kuadhimisha siku ya kuzaliwa kwake. Sherehe iliyofanyika nyumbani kwao. Kwa hivyo wimbo huu una urudiaji wa sauti “furaha tele kwako-oo”. Kwa maana hii basi kusisitiza maana ya hafla hiyo. Kuna aina nyingi za takriri, lakini lengo letu ni kubainisha tu uwepo wa mbinu hii katika matini tunayoichambua wala si kuzichanganua takriri.

**3.1.3.4 Tasfida**

Kwa mujibu wa NJogu na Chimera (1999) wanasema kuwa tasfida ni mbinu ambayo hutumia lugha safi ili maneno machafu yasitumike. Tasfida pia huitwa tauria na hutumiwa kwa lengo la kukwepa fedheha na hivyo humwezesha msanii kuandika au kusema hoja “Chafu” mbele za watu bila kuchukiza au kufanya moyo wa msomaji na msikilizaji utibuke. Matumizi ya maneno machafu inadhihirisha uozo wa adabu katika lugha.

Wamitila (k.h.j. uk. 194), anadai kwamba “tasfida ni matumizi ya maneno ya kupunguza ukali au uzito fulani”. Mahali pakutumia lugha inayokera au matusi, kutumia lugha inayoficha makali hayo.

Hii ni mbinu itumiwayo katika hali za kutaka mambo yasiyotakikana kusikika yasemwe kwa njia inayokubalika. Hutumika kupunguza makali ya jambo linalosemwa. Mfano

ufuatao unadhihirisha maelezo yaliosemwa: *Tayari Bibi,* (uk. 3) Hii ni kauli iliyosemwa na Bob kumwambia Vera mwanamke wa Kizungu kuwa amemaliza kuliosha gari. Kwa hiyo neno "Bibi" linaonyesha adabu aliyonayo Bob kwa kumwita Vera hivyo.

Mifano mingine ifuatayo bado inadhihirisha dhana ya tasfida.

> *Wasichana….Ingawa walikatazwa kucheza nasi kwa sababu wengi wao walikuwa washavunja ungo*. (uk. 26).

Hapa wasichana na wavulana wa rika moja, katika kituo cha polisi cha Bondeni, walikuwa wanacheza pamoja. Lakini baada ya kukua na kubadilika kimwili, wanashauriwa kucheza sehemu tofauti. Wavulana kwao na wasichana sehemu yao. Hivyo basi, usemi "kuvunja ungo" ni tasfida kuashiria kuwa wasichana wanaweza kupata mimba ikiwa watashiriki ngono na wavulana,

> *Mama wee!" Jamila alitoa kilio na kunikumbatia kwa nguvu mlango ulipofunguka. Ndipo tuliposhika njia kuu na kufululiza chapuchapu kwa raha isiyokadirika.* (Uk. 62).

Tumeona kuwa Jamila anampa Bob zawadi yake kama alivyomuahidi. Usemi huu unaonyesa tendo la mapenzi baina ya wapenzi hawa wawili. Tendo hili limeelezwa kwa lugha ya heshima sana, na huu ndio utasfida wa lugha, msomaji hawezi kukerwa au kuchomwa na maelezo haya.

> *……..unakutana nao kwa uhitaji tu* (uk.160).

Maneno haya yalisemwa na Jamila akimwambia Bob kuhusu Vera mwanamke wa Kizungu na Gaceri. Jamila yuko masomoni na anaona pengine Bob mpenzi wake anafanya ngono na wengine (Vera na Gaceri). Kwa hivyo kauli hii inaonyesha matumizi ya tasfida katika lugha. Tumesema kuwa tasfida ni njia ya matumizi ya lugha kwa njia ya heshima na isiyokera msomaji au msikilizaji.

#### 3.1.3.5 Nidaa

Kulingana na Mugambi (1992:134) anasema kuwa mbinu hii ni *Kama namna ya msemo wa mawasiliano au sauti ya mshangao aitumiayo msanii kudhihirisha maoni yake ya ndani*. Msemo huu waweza kutoa hisia za ndani za mhusika kwa kutoa sauti ya kilio ambacho chaweza kuwa cha mshangao, huzuni, furaha au chuki.

*Vipanya vya Maabara* ina mifano ya baadhi ya mbinu hii, nayo ni:-

*Aisee Bob! (uk. 6).* Ni kauli iliyosemwa na mlinzi akimwita Bob. Pengine mlinzi alikuwa akitaka kitu fulani kwake.

*Kiasi kikubwa! (uk. 13).* Hali ya mshangao alionao Bob juu ya Swaleh kukodisha bunduki ili akaibe. Kwa hivyo Bob anashangaa kwa pesa zitakazolipwa.

*Wairi! Hodari sana kwa kuwastarehesha wateja wake(Uk 13)* Ni wakati Bob anamtembelea Wairi kwake, Swaleh anamdhihirishia Bob kuwa kweli Wairi anaifahamu hali ya kufanya mapenzi sawa sawa.

*Waai Ongeti! Bwanangu Ongeti!* (uk. 145) .Hapa nidaa imetumika kuonyesha huzuni. Kelele hizi zilikuwa zikifanywa na Ongeti wakati mumewe  ameaga dunia hospitalini Kenyatta. Ni kelele za uchungu. Hali hii inamfanya msomaji kuhisi vile mhusika anavyohisi na pia jinsi msomaji atakavyo hisi kuhusu mhusika huyo.

*Alistahili adhabu hiyo! (uk. 59)* Haya ni mawazo yaliyotolewa na marafiki wa Wairi walipopata habari za kuwa mwalimu mkuu aliyemtunga mimba Wairi anastahili adhabu

kali. Katika riwaya ambayo tumeichanganua, mbinu hii ya nidaa imetumika kwa wingi. Na matumizi yake yanamweka msomaji kuyafuata yanayosimuliwa na kuathirika.

**3.1.3.6 Tashihisi**

Tashihisi ni tamathali ya semi ambayo vitu au wanyama hupewa sifa zote au baadhi ya sifa za binadamu. Kuna mifano mingi katika V*ipanya vya Maabara*. Mbinu hii imetumika ili kuzidi kumfanya msomaji kupata mawazo ya ndani ya habari au matini aisomayo. Pia inampatia hamu ya kutaka kuendelea kufahamu yatakayojiri baadaye.

Mifano hii ifuatayo inabainisha mbinu hii. *Majengo makuu yalisimama kwa msongamano kama kwamba yalikuwa yaking'ang'ania nafasi ndogo* (uk.8). Majengo hapa yamepewa uhai kama kwamba yanasema au kuzungumza. Kauli hii inaonyesha vile majengo yalivyo karibu au kushikana kwa jinsi yalivyo mengi.

*Macho yangu yaliposhiba muujiza uliozuliwa na mataa ya …*(uk. 8) Macho yamepewa uhai wa binadamu. Kuwa pengine yalikuwa yameshiba muujiza uliokuwa ukionekana.Hali hii inamfanya msomaji kutafakari zaidi juu ya yale yanayosimuliwa.*Upande wa kulia kulikuwa na safu ya milima iliyobeba miamba mikubwa mgongoni(uk 154.)* Hapa milima imepewa uhai. Inaonekana juu ya milima kulikuwa na miamba ya mawe. Huo ni uhuishaji mzuri sana.

*Niliona majabali meusi yaliyotapakaa katika sehemu kubwa na kuumeza mto (uk. 155).* Majabali meusi yamepewa sifa za binadamu kuwa yana uhai na kuwa yanaumeza mto.

Kumaanisha kwamba majabali haya yanaufifiza mto yaani kuuangamiza. Msomaji anaweza kuwa na maswali mengi juu ya majabali haya. Yatawezaje kuumeza mto? Bila shaka hayawezi, njia hii inamfanya msomaji kukuza uwezo wake wa kudadisi na kufikiria mambo.

### 3.1.3.7 Kuchanganya Ndimi

Kuchanganya ndimi ni mbinu ambayo hutokea wakati mzungumzaji anatumia lugha mbili wakati wa mazungumzo. Pia hali hii huonekana katika matini za fasihi pale ambapo mwandishi, kupitia kwa wahusika wake watatumia na kuchanganya aidha maneno na sentensi za lugha mbili au zaidi. Endapo wanazungumza Kiswahili wanaweza kutia maneno ya Kizungu. Mbinu hii inaonyesha jinsi mtu alivyo katika umilisi na ufahamu wa lugha zaidi ya moja. Pia huonyesha uhodari wake wa utumizi wa lugha. *Vipanya vya Maabara* imeonyesha mbinu hii. Mbinu hii basi inamweka msomaji kufahamu jinsi wahusika walivyo na ujuzi wa lugha kadhaa.

Mifano ya mbinu hii ni:

“Sasa *Darling*? (uk 6)
*Darling* kumaanisha kipenzi au mpenzi
Wazungu walichokiita dignity (uk 78)
*Dignity* kumaanish hadhi
“*Anyway*, nitakupa bia mbili kwa leo” (uk 81)
“*Anyway*” kumaanisha hata hivyo.
…. Kama *Yule basket baller wa US* (uk 90)
*Basket baller* inamaanisha mchezaji wa mchezo wa vikapu.
U.S, inamaanisha muungano wa *Taifa la Marekani*
Yule *Black American* (uk 91)
*Black American* ni mwamerika mweusi
Huo mpango *wa retrenchment* (uk 217)

*Retrenchment* kumaanisha ustaafishaji wa wafanyakazi kwa hiari.

Mbinu hii huifanya kazi ya kifasihi kuwa na mnato na kumfanya msomaji kuwa makini.

**3.1.3.8 Methali**

Methali ni sanaa ya lugha iliyo na maana fiche inayostahili kufumbuliwa na msomaji au msikilizaji. Ni matumizi ya lugha kwa ufundi unaoweza kumwathiri msomaji kifikra.

Andambi, na Murono (2005) wanasema kwamba, methali zina malengo mbalimbali kama vile kushauri, kushutumu, kuliwaza, kupongeza na kuonya. Tukiongezea, methali ni kiungo mmojawapo cha kuipamba lugha. Matumizi mazuri ya methali kwenye matini ya kifasihi ni tunu, kwani huifanya ipendeze na kupendwa.Katika riwaya tunayoichanganua, mbinu hii imetumika vizuri tena sana.

Hapa kuna baadhi ya mifano ya methali ipatikanayo katika *Vipanya vya Maabara*.

*Avumiliaye huja kula mbivu (uk. 20).*Ni methali iliyosemwa na kinyozi kumtia moyo Konstebo Kerogo kuwa azidi kufanya kazi ya polisi na siku moja atapandishwa cheo.

*Fadhili za punda*…. (uk.34). Ni methali iliyoachwa wazi ili wengine wakamilishe kwa kusema ni mashuzi. Okach aliwatania wenzake.

*Dau la myonge haliendi joshi* (uk.44). Methali aliyoisema Konstebo Kerogo kwa bintiye Freda. Kwa kuwa ni maskini basi hawawezi kuendelea maishani na Freda hawezi kuendelea na masomo yake, ambavyo sivyo. Binadamu anatakikana asikate tamaa kabisa maishani. Pengine mwandishi anataka kutuchorea picha kuwa ulimwenguni wako watu

wa aina ya mhusika huyo. *Nazi mbovu miongoni mwa walimu zilikuwa harabu kwa sifa nzuri ya kazi hii[* uk. 88]. *Nazi mbovu harabu ya nzima,* ndivyo hasa methali ilivyo. Mwandishi ametaka kutuonyesha ufundi wa hali ya juu na ambao ni wa kisanaa. Ni sharti msomaji awe makini sana ndipo afahamu kuwa ni methali. Labda ni mbinu ya mwandishi kumshirikisha msomaji katika kazi yake.

*Kipendacho moyo ni dawa[ uk 114].* Bob alimwambia Swaleh methali hii, kwa vile kila mmoja anacho akipendacho zaidi. Bob apenda kutafuna miraa ilihali Swaleh anapenda kunywa pombe. Hapa tumechorewa uraibu wa marafiki hawa wawili.

*Umoja ni nguvu utengano ni udhaifu* (uk. 139). Hapa ni wakati ambapo Okach anatoa hotuba mbele ya wenzake wakati wa sherehe ya kuadhimisha kufuzu kwa Freda masomo yake ya utawa na uuguzi. Anawaambia wenzake kuwa wakiwa na umoja katika kutenda jambo lolote lile watafanikiwa. Inaonekana Okach ni mhusika mwenye maarifa na msemaji hodari. Kutokana na hali zake za uzungumzi, kuna mteka msomaji na kumfanya azingatie yasemwayo na mhusika. Kwa hiyo mbinu ya methali imekuwa kiungo muhimu katika ujenzi wa riwaya hii.

### 3.1.3.9 Ritifaa

Neno ritifaa ni istilahi ya kigiriki yenye maana ya “kwenda mbali”. Hii ni tamathali ya usemi ambapo mwandishi na hata mzungumzaji huelekeza usemi wake kwa mtu wa kufikirika, kitu au sifa ya kidhahania. Mbatia (2001:70) anaiangazia ritifaa kama mbinu ambapo mtunzi au mhusika anaongea na mtu au kitu kisichokuwepo ili kutoa hisia, fikra

au mawazo yake kuhusu kitu hicho. Kitu kinaweza kuwa kiumbe cha kuaminika tu kama malaika, Mungu, kizuu, mzuka au kitu chochote kisicho na uhai. Mfano, mhusika katika kazi ya kifasihi anaweza kuzungumza na mlima au msitu kama anavyoongea na binadamu. Naye mtu anaweza kuongea na mtu ambaye hayuko kana kwamba mtu huyo yuko.

Ritifaa ni mbinu ya kitamathali ambayo ina mwelekeo mkubwa wa kisaikolojia na huweza kujitokeza kama uzungumzi nafsi ndani. Kwa hali hii, ritifaa hudokeza mawazo na hisia za kindani za mhusika. Mbinu hii hulenga kuibua hisia kwa msomaji na kwa hivyo, huwa na athari yakisaikolojia.

> *Mfano. Lakini kulitokea nini humo garini? Lile vurugu na unyende vilimaanisha nini? kwa nini waziri alimburura kutoka kiti cha mbele cha gari na kumlaza ndani ya buti?(uk 171)*

Mawazo haya yalikuwa yakimpitikia Bob akilini mwake. Ni wakati alipomwona waziri Rashid Hamisi akimnyonga Rita Kingi (jasusi). Baadaye waziri alimburura na kumlaza marehemu Rita Kingi ndani ya buti.

Rashid Hamisi alifanya hivyo ili kuficha ushahidi.

Ritifaa inachangia katika ujenzi wa ploti kuu ya kazi hii. Vile vile inautilia nguvu ujumbe mkuu wa kazi.

### 3.1.4: Jinsi mawazo yanavyowasilishwa katika *Vipanya vya Maabara*

Hizi ni mbinu za kimtindo ambazo mwandishi anazitumia kuyadokeza tu mawazo ya wahusika katika kazi za kifasihi. Kulingana na Leech na Short (2007:270) uwasilishaji

wa mawazo unatuwezesha kuyajua mawazo ya mwandishi na wahusika. Hapa itategemea mbinu inayotumiwa kuwasilisha mawazo. Mbinu hizi za kuwasilisha mawazo ni uwasilishaji halisi wa mawazo, uwasilishaji halisi huru wa mawazo, uwasilishaji taarifa huru wa mawazo pamoja na ripoti ya usimulizi wa tendo la mawazo. Mbinu hizi za uwasilishaji wa mawazo husaidia kutoa fununu fulani ya madhumuni ya matendo ya wahusika, fikra, misimamo na habari zinazowahusu – wasifu. Kwa mkondo huu basi tunaweza kufahamu ujuzi na ung'amuzi wa mawazo yao. Sisi tumeangazia mbinu mbili za uwasilishaji.Hizi ni uwasilishaji halisi huru na uwasilishaji halisi.

**3.1.4.1 Mtindo wa uwasilishaji halisi huru wa mawazo**

Kulingana na Leech na Short (k.h.j) njia hii inatofautiana na uwasilishaji halisi wa mawazo kwa kuwa hauna kitangulizi chochote cha taarifa. Toolan (1998) anasema kwamba huu ni uwasilishaji wa mawazo ambapo kuna mtiririko huru wa mawazo halisi ya mhusika bila ya kuwa na alama za kunukuu. Sisi tumeona kuwa mbinu hii inadhihirisha mawazo yaliyo hai ambayo yanampata mhusika. Mawazo hayo yanawasilishwa kama muundo fulani wa usemi. Njia hii ya uwasilishaji, inabainisha mawazo halisi ambayo yanampitikia mhusika, hivyo kumwathiri kisaikolojia. Pia mhusika huweza kueleza hisia zake kikamilifu.

Mbinu hii inapotumika katika kazi za kifasihi, huweza kusaidia kubainisha msimamo na fikra za mhusika mmoja na mwingine. Kutokana na hali hiyo tunaweza kuonyesha mambo yanayowapitikia akilini na hata katika maisha yao.

Mbinu hii ya uwasilishaji halisi huru wa mawazo inaonekana sana katika *Vipanya vya Maabara*. Labda mwandishi amehiari kutumia mbinu hii kuakisi hali za wahusika kisaikolojia. Mfano huu unadhihirisha mbinu hii ya uwasilishaji. *Kimya kilitawala tena. Niliona kuwa maneno ya mjomba yalikuwa makali lakini yenye busara. Yalielekea kukubaliana na yale ya Freda aliyomwambia baba asubuhi* (uk. 52).

Haya ni mawazo yaliyo hai katika ung'amuzi wa Bob hasa kumhusu babake. Yaliyosemwa na Freda kumwambia babake Kerogo, yalikuwa sawa na yale yaliyosemwa na mjomba wao Mbaabu – haya ni mawazo hai na halisi ya mhusika. Kutokana na kifungu hiki tunaweza pia kupata hisia za ndani za mhusika.

**3.1.4.2 Mtindo wa uwasilishaji halisi wa mawazo**

Mtindo huu wa uwasilishaji wa mawazo hurejelea usemi uliotamkwa na mhusika au wahusika bila kuufanyia mabadiliko yoyote yale. Alama za kunukuu hutumika na huweza kuambatana na kitangulizi cha usemi husika. Leech na Short (k.h.j) wamesema kwamba kiambishi cha nafsi ya kwanza – ni-cha umoja au tu-cha wingi hutumika katika njeo iliopo.

Fikra zinazojibainisha katika mtindo huu ni ya mhusika. Kwa hivyo tunaweza kubainisha anavyowaza na pia anavyohisi. Mbinu hii basi ndiyo mhimili na nyenzo kuu kabisa ya dayalojia. Hivyo basi matumizi yake huifanya kazi ya kifasihi hasa ya kinathari kuwa hai.

Katika V*ipanya vya Maabara* mbinu hii imetumika sana na kuakisi mazungumzo ya wahusika katika riwaya hii. Hapa kuna mfano mzuri wa mazungumzo kati ya Bob na Jamila.

> *"Mapenzi yangu kwako Jamila sio kitu ninachoweza kukieleza. Nakupenda kwa moyo wangu wote. Hata "sijui nisemeje mpenzi."*
> *"Waitaka zawadi yangu?"*
> *Naitaka. Naitaka sasa hivi" (uk. 61-62).*

Katika sehemu hii ya mazungumzo, tunaona kuwa Bob anaonyesha kuwa na uhuru wa kumwambia mwenzake kuwa anampenda sana. Jamila kwa upande wake yuko tayari kwa mapenzi ya dhati. Kutokana na swali lake, tunaona kuwa kweli Jamila anataka kumpa Bob zawadi yake ya mapenzi. Tumeona kuwa kutokana na wanayoyazungumza, tunapata mawazo na hisia zao kuhusu mapenzi na hata msukumo wa kukutana pamoja.

**3.2 Hitimisho**

Sura hii ya tatu tumezungumzia juu ya mtindo kama njia ya kujieleza kilugha na kisanii. Kulingana na uhakiki huu, tumechunguza tu vipengele vinne vya mtindo. Hivi ni pamoja na, italiki, tamathali ya lugha, jinsi mawazo yanavyowasilishwa na sintanksia.

Tumeona kuwa sintaksia inamsaidia na kumfanya msomaji kuwa na uzingatifu ufaao kusudi apate maana inayojibainisha katika sentensi. Njia hii pia huweza kuonyesha mkururo wa mawazo ya wahusika. Kwa upande mwingine, italiki imetumika kama njia ya kusisitiza maneno pamoja na vifungu fulani ili msomaji wa matini husika avipe uzingatifu zaidi. Lugha ya kitamathali imetumika sana katika *Vipanya vya Maabara*.Katika sehemu hii tumechunguza tu mbinu kadhaa ambazo ni maswali ya

balagha, tashbihi, nidaa, takriri, methali, tashihisi, kuchanganya ndimi na ritifaa na tasfida. Nazo mbinu za uwasilishaji wa mawazo zimejibainisha katika riwaya hii, ambazo ni uwasilishaji halisi huru wa mawazo na uwasilishaji halisi wa mawazo. Kwa maoni yetu tumeona zimefaulu kusawiri hali za wahusika.

Kwa hivyo ni bayana kuwa mtindo umesukwa na kutumika kiustadi kudokeza hali za wahusika. Mbinu hizi za kimtindo zinaonyesha ukuaji wa kimtindo katika riwaya ya Kiswahili kwa kasi.

# SURA YA NNE

# HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 4.0 Utangulizi

Sehemu hii ni hitimisho la utafiti wetu. Pamoja na hayo, tumetathmini uhalali wa nadharia tete kwa kubainisha kama kweli zilifaa na kutimizwa. Zaidi ya yote tumetoa mapendekezo kwa wasomi, watafiti na wahakiki wa siku za usoni kwa jumla kuhusu yale yanayoweza kuwafaa na kuwasadia kufanya utafiti zaidi kuhusu riwaya ya Kiswahili.

## 4.1 Muhtasari wa Matokeo

Baada ya kuichanganua *Vipanya vya Maabara* na tukiizingatia kimtindo,

Tumegundua kuwa, *kazi hii* ni riwaya ya kisasa. Kwani msanii amewahusisha wahusika wake na maswala ya ulimwengu wa sasa. Mwandishi ameweza kuweka msisitizo mkubwa katika uhusika wa ndani. Kwa maana hii wanajitokeza wahusika wanaoumia ndani kwa ndani kama vile Konstebo Kerogo. Zaidi ya hayo, kuna mbinu za kisaikolojia ambazo zimetumiwa kuunda msuko wa kazi hii kama usimulizi nafsia ulio na upenyezi wa mawazo pamoja na hisia za wahusika kwa kutumia usimulizi wa nafsi ya kwanza na pengine ya tatu.

Tumeona kuwa kuna mbinu za kimtindo zilizotumiwa na mwandishi kwa lengo la kumwathiri msomaji kisaikolojia. Baadhi ya mbinu za mtindo zilizotumiwa ni matumizi ya italiki, lugha ya kitamathali, njia za uwasilishaji mawazo pamoja na sintaksia yenye nyufa. Matumizi ya mbinu hizi yanadokeza mawazo na hisia za wahusika hivyo basi

zinamwongoza msomaji kwenye mkondo wa fikra za wahusika. Kwa mantiki hii, msomaji anaweza kuwazia wahusika wanavyowaza na pia ahisi wanavyohisi. Kwa jumla, msomaji huenda akaathiriwa na mfumo mzima wa uwasilishaji wa mawazo kama alivyofanywa mwandishi.

Kwa maoni yetu, mwandishi amefaulu kutumia kunga za kifasihi kadri ya uwezo wake. Hata hivyo, tumeona kuwa ametumia tashibihi kwa wingi zaidi ya kunga nyingine.

Wanamuundo wanaviona vipengle vya fani kama viashiria na maana inayotokana na vipengele hivi vya kimtindo ndivyo viashiriwa. Kwa hivyo tumeweza kusema kuwa vipengele vya kimtindo ni baadhi ya nyenzo zinazounda fani katika matini ya kifasihi. Wanamuundo wanasema kuwa kufaulu kwa kazi ya kifasihi hutokana na mbinu za mtindo ambazo msanii anazitumia. Hoja hii ni ya kweli tukirejelea *Vipanya vya Maabara*. Mwandishi wa riwaya hii ameonyesha ufundi wake kwa kutumia mtindo kwa ustadi wa hali ya juu.

Nadharia hii imetufaa sana katika utafiti wetu. Imetupa mwongozo wa kuridhisha wa kuchanganua baadhi ya vipengele vya mtindo. Mwisho, nadharia hii ikifuatwa na waandishi wengi wa kazi za fasihi, bila shaka kazi hizi zitawavutia sana wasomaji na kuathiriwa kwa njia mbali mbali kutegemea na mitazamo yao.

### 4.2Upimaji wa nadharia tete

Utafiti wetu uliongozwa na nadharia tete tatu. Mosi, kuwa vipengele vya kimtindo vilivyotumika katika *Vipanya Vya Maabara*vimechangia pakubwa katika uwasilishaji wa maana katika riwaya hii. Kulingana na uchanganuzi na ugunduzi wetu, nadharia tete hii imetimizwa. Sababu ni kuwa ili riwaya iwe ya kuvutia na ifikie upeo wa juu, basi vipengele vya kimtindo sharti vitumike sawasawa. Katika kazi hii kama ilivyo katika riwaya nyingine, huwa kuna wahusika ambao wameumbwa kudokeza tu hali zao za kutatizika ndani kwa ndani na kukosa matumaini maishani. Vivyo hivyo kazi hii imesukwa kwa mbinu zinazoifanya riwaya ya kuvutia. Uzungumzi nafsia na dayalojia baina ya wahusika ni baadhi ya mbinu zilizotumika.

Mbinu hizi zimetumika kuonyesha wahusika na matendo yao. Hivyo basi kuweza kuwasilisha maana katika riwaya na kumfanya msomaji kuweza kuyafahamu na kuyaelewa matendo ya wahusika. Matumizi mapana ya maswali ya balagha, tashbihi, italiki, nidaa, takriri, tasfida na nyenzo nyingine zimetumika kudokeza mawazo na hisia za wahusika ambao ndio hujenga riwaya. Na kwa njia hii basi kuzidi kuwasilisha maana katika riwaya hii.

Nadharia tete yetu ya pili inasema: msanii wa *Vipanya vya Maabara* amefaulu kupitisha ujumbe kwa mnato kutokana na mtindo aliotumia. Tumethibitisha nadharia tete hii kwani kwa hakika mwandishi amefaulu kupitisha ujumbe kwa kutumia vipengele vya kimtindo ipasavyo. Tumeona vile ametumia tamathali za usemi kama tashbihi, ambazo zimetumika sana na kwa njia nzuri. Uchanganyaji ndimi, maswali ya balagha, italiki, uzungumzi wa ainaaina, matumizi ya sentensi zisizokamilishwa (mapengo), wahusika

wengi wakiwa vijana ni kati ya vipengele ambavyo msanii amevitumia kwa njia iliyojenga umbuji katika riwaya hii.

Nadharia tete yetu ya tatu ilidadisi endapo msanii amefaulu au amefeli, kulingana na vipengele vya mtindo alivyotumia. Maoni yetu kuhusu nadharia tete hii ni kuwa, msanii amejitahidi kutumia vipengele vya mtindo kwa njia bora hivyo basi, amefaulu. Tumesema kwamba, tashbihi zimetumika zaidi. Pengine kwa kuwa mwandishi aliona kunga hii kuwa mwafaka zaidi katika kuzibaini sifa na hulka za wahusika wake katika riwaya hii.

**4.3 Mapendekezo ya utafiti zaidi**

Katika utafiti wetu tumejikita katika uhakiki wa baadhi ya vipengele vya mtindo katika riwaya hii kwa kutumia Umuundo. Kuna haja ya kutafiti juu ya vipengele vya kidhamira ambavyo hatukuvichunguza kama maudhui,swala la jinsia na mengine.

## MAREJELEO


Crystal, D. na Davy, D. (1969) *Investigating English Style*. Longman Publishers.

Frye, N. Baker, S. na Perkins, G. (1985) *The Harper Handbook of Literature.* New York: the Harper Collins. College publisher.

Henderson, G. Day, W. na Waller, S. (1994) *Literature and Oursevles*. New York: Harper Collins College – Publishers.

Holman, C. H. (1976) *A Handbook of Literature.* Indianapolis*:* The Odyssey Press.

Indangasi, H. (1988) *Stylistics,* Nairobi: Nairobi University Press.

Kimani, N, na Chimerah R. (2008) *Ufundishaji wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Kirumbi, W. (1975) *Fani ya Nyimbo katika Fasihi Simulizi.* Tasinifu ya M.A Chuo kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).

Kisilu, P. N. (2003) "Mwingiliano wa Fani na Mudhui Katika Ushairi wa Kithaka Wa Mberia". Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu Cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Kitsao, J. (1975) A Stylistic Approach Adopted for the Study of Written Swahili Prose Texts. Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu Cha Nairobi. Haijachapishwa).

Leech, G. na Short, M. (2007) *Style in Fiction: A Linguistic Introduction to English Fictional Prose* (Tol. 2) Harlow: Longman.

Marwa, B. Mariam (1987) *Uchambuzi wa Mtindo Baina ya Ngano za Waswahili na Wakuria.* Tasnifu ya M.A. ya Chuo Kikuu Cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Mathews, P. H. (1997) *Oxford Concise Dictionary of Linguistics.* Oxford: Oxford University Press.

Mazrui A. (1981) *Uchambuzi wa Riwaya*. Nairobi. Kenya.

Mazrui, A. na Syambo, B. (1992) *Uchambuzi wa Fasihi.*Nairobi: East African Educational Publishers.

Mbatia, M. (1999) The origin and development of the Swahili Thesis novel in Tanzania: Tasnifu ya Uzamifu chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).

__________ (2001) *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi: Standard Textbook Group and Publishing.

__________ (2007) *Vipanya vya Maabara*. Nairobi. Jomo Kenyatta Foundation.

Mboti, D. (2012) "Mtindo Katika Nyimbo za Michezo ya Watoto wa Darasa la Kwanza Katika Tarafa ya Starehe Nairobi". Tansifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).

McIntosh (1963) *Language and Style in Sociolinguistics,* Pride, J. B. na Holmes Penguin Books.

Mgullu, R. S. (1999) *Mtalaa wa Isimu:*Nairobi. Longhorn Publisher Ltd.

Mlacha, S. A. K. (1995) *Dhima ya Methali katika malezi*. Tuki: Dar es salaam.

Mlacha, S. na Madumulla J. (1991). *Riwaya ya Kiswahili*. Dar es salaam.

Mohamed, S. A. (1990) *Kunga za Nathari ya Kiswahili*. Nairobi. E.A.P.H.

Msokile M. (1992) *Misingi ya Hadithi Fupi. Dar-es-salaam*: Dar es Salaam.

_________ (1993) *Msingi ya Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi. E.A.E.P LTD.

Mogambi, H. (1992) *Uhakiki wa Maudhui katika Tamthilia za Kiswahili*. Tasnifu ya M. A. Chuo Kikuu Cha Nairobi (Hijachopishwa).

Mugwika, K. Ferinda (2012) "Dhana Ya Uchimuzi Katika Uendelezaji wa Riwaya ya Kimajaribio ya Mafamba". Tasnifu ya M.A. ya Chuo Kikuu Cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Mukhata, C. (2011) Uhakiki wa mtindo katika *Nyuso za mwanamke*: Tasnifu ya Uzamili: Chuo Kikuu Cha Nairobi (Haijachapishwa).

Mulokozi, M. M. (1989) *Tanzu za Fasihi*-Mulika 21. Dar es salaam.

Mweri, J. (2010) *Utangulizi wa Isimu*: Nairobi. K.L.B.

Naliaka, Ruth (2012) Hali ya Vijana Katika Riwaya ya *Vipanya vya Maabara*. Tasnifu ya M.A. ya Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Ngure, A. (2003) *Fasihi Simulizi*, Nairobi. Phoenix Publishers.

Njogu, K. na Chimera, R. (1999) *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Okondo, K. na Wacira, D. (2012) *Effective Composition writing for Primary Schools Kenya*: Oxford University Press.

Omwoyo, O. (1997) *Fani katika ushairi wa Hassan Mwalimu Mbega: Uhakiki wa Upisho wa Malenga*. Tasnifu ya M.A. ya Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Ruo, K. R. (1989) *Tamathali za semi kwa wanafunzi wa Kiswahili*. Nairobi. Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Shaw, H. (1972) *A Dictionary of Literary Terms.* New York: MacGraw Hill.

Swaleh, A. (2011) A Critique of the Mapping and Construction of Gender Identity and Authority in Selected Kiswahili Novels. Tasnifu ya uzamifu: chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).

T.U.K.I (1990) *Kamusi ya Kiswahili*, Dar es salaam Oxford University Press.

_________(2000) *English–Swahili Dictionary* Dar es Salam: Institute of Kiswahili Research.

___________(2004) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* 2nd edition. Dar es salaam. Oxford University Press.

_________(2013) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu. Toleo la 3*. Kenya: O. U. P

Toolan, M. (1998) *Language in Literature. An Introduction to Sytlistics.* London: Arnold.

Wamitila K. W. (2002) *Uhakiki wa Fasihi, Misingi na Vipengele Vyake*. Phoenix Publishers Ltd.

____________ (2003) *Kamusi ya Fasihi Isitilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publication.

____________ (2003) *Kichocheo cha Fasihi simulizi na andishi.*Nairobi: Focus Publication.

____________(2008) *Msingi wa Uchanganuzi wa Fasihi*. Vide – Muwa. Nairobi: Focus Publication.